

SHERHE YA KITABU

**AL-USULU – THALATHA NA DALILI ZAKE
(MISINGI MITATU YA IMANI)**

BISMILLAH RAHMAN RAHIM

Kwa hakika kila sifa njema ni milki yake **Allah**. Nasi tunamsifu na tunamuomba msaada na tunamtaka msamaha, tunajilinda kwa **Allah** na shari zote zitokanazo na nafsi zetu na ubaya wa matendo yetu.

Yeyote ambaye ameongolewa na **Allah** basi hakuna yeyote atakae mpoteza na yule aliyempoteza hakuna wa kumuongoa.

Ninashahadia ya kwamba hakuna anayestahiki kuabudiwa ila ni **Allah** pekee asiye na mshirika Na nashuhudia ya kuwa **Muhammad** swalalahu walaih wasalam ni mja wa **Allah** na mtume wake.


Ama ba'ada

YALIYOMO.

AL-USULU – THALATHA NA DALILI ZAKE.

NO.	MAUDHUI	UKURASA
1	UTANGULIZI	
2	MAMBO MANNE YA MSINGI	
3	MAMBO MATATU YA MSINGI	
4	UMUHIMU WA KUSOMA TAUHID	
5	AL-USULU – THALATHA	
6	HITIMISHO	
7	MUHTASARI YA SHERHE YA KITABU	
8	MAZOEZI YA AL-USULU THALATHA NA DALILI ZAKE	


UTANGULIZI:



SABABU YA KUKICHAGUA KITABU HIKI KUWA CHA MWANZO KATIKA KUJIFUNZA (TAUHID)

- Ni kushughulika waja wema waliotangulia na wanachuoni wetu katika ahlul sunna waljamaa kukifundisha kitabu hichi kilichobarikiwa kutokana na yale yaliyomo ndani yake katika manufaa na faida kubwa ambazo zimekifanya kitabu hiki kuwa ni msingi atakaoutumia mwanafunzi na atajenga juu yake paa lake zima la elimu ya kisheria, basi kwa hali hiyo na sisi tunawafuata waja wema waliotangulia na tunapita kwenye nyendo zao katika kufuata mfumo huu (wa kuanza na kitabu hiki kujifunza).
- Na kama ilivyo pia kwa watu wote hawatajitosheleza na elimu hii ya (Tauhid) kabla ya kukisoma kitabu hiki na maudhui zote zilizo ndani yake zinazoeleka misingi ambayo ni lazima kila muumini aiadini kwa imani ya kweli isiyo na chembe ya shaka yoyote.

UBORA NA UPEKEE WA KITABU HIKI ALICHOKIANDIKA MTUNZI WAKE
(Allah amrehemu)



KUITAMBUA MISINGI MITATU YA IMANI.

Kwa ufupi misingi mitatu ni yale maswali matatu atayoulizwa mtu kaburini.

1. Nani Mola wako?

2. Ipi dini yako?

3. Yupi Mtume wako?

Ni nusra ipi tutakayoipata ikiwa tutaisoma hii misingi?

Bila shaka yoyote utakapoisoma hii misingi mitatu, kisha ukaifanyia kazi na ukailingania kwa wengine, ikiwa umefanya subra katika kusoma, kutenda na kulingania biidhinillahi utayajibu maswali haya kaburini

YALIYOMO KWENYE KITABU HIKI CHA MISINGI MITATU:

Kitabu hiki kimegawanywa katika sehemu kuu tano nazo ni:-

1. MAMBO MANNE YA
MSINGI KATIKA
SURATUL-ASRI

2. MAMBO MATATU YA
MSINGI KWENYE
VIGAWO VYA
TAUHID

3. UMUHIMU WA
KUJIFUNZA ELIMU
YA TAUHID

4. MISINGI MITATU YA
IMANI (MASWALI YA
KABURINI)

5. HITIMISHO

1. MAMBO MANNE YA MSINGI

1. Kutafuta elimu

2. Kuifanyia kazi
elimu

3. Kulingania elimu
hiyo

1. Kuwa na subira kwa
maudhi yote wakati wa
kulingania

2. MAMBO MATATU YA MSINGI

2. Tauhid Rububiya na
Tauhid Asmai wa
sifati

3. Tauhid Uluhiya
(Tauhid ya ibada)

4. Kujitenga mbali na shirki na
wenye kufanya shirki (kwa
kutumia ulimi, moyo na viungo)

3. MUHIMU KUJIFUNZA TAUHID

Hili ni jawabu la swali hili: Kwanini tunajifunza Tauhid?

4. MISINGI MITATU

Kwa ufupi misingi mitatu ni maswali matatu ya kaburini

Ni nani Mola wako

Ni ipi dini yako

Nani Mtume wako

5. HITIMISHO

Ni kuanzia kauli ya mtunzi wa kitabu Allah amrehemu
“WATU WATAKAPOKUFA WATAFUFULIWA TU” mpaka mwisho
wa kitabu hiki.

JAMBO LA KWANZA

MAMBO MANNE YA MSINGI:

Bismillah Rahman Rahim.

Tambua ewe Muislamu **Allah** akurehemu inakupasa kujifunza mambo manne ya msingi:

1. Kutafuta elimu nako ni kujifunza kumjua **Allah**, na Mtume wake (*swalla llahu alayhi wasallam*) na kuijua dini ya Uislamu kwa dalili.
2. Kuifanyia kazi elimu (baada ya kusoma)

HIZI NDIZO SABABU ZA MTUNZI KUANZA KWA BISMILLAH

1. Ni kwaajili ya kukifuatisha kitabu cha Allah (Qur'an) na kuwaiga Mitume (rehema na amani ziwe juu yao)

2. Kuwaiga waja wema na wanachuoni waliopita ambao ilikuwa ni ada yao kuanza na Bismillah katika utunzi wa vitabu vyao

3. Pia ni katika mlango wa kutabaruku kwa jina tukufu la Allah aliyetukuka.

Kama tulivyoonesha kwenye utangulizi ya kwamba ilikuwa ni ada ya Sheikh Mtunzi wa kitabu kuanza kwa kuwaombea dua wanafunzi na kuwaombea kwa Allah awarehemu na kwa ibara ifuatayo ni ushahidi tosha juu ya hilo.

Huruma ya wanachuoni wa Ahlu Sunna waljamaa ipo kwa wanafunzi wao, nayo ni kwa sababu dini ya Uislamu imejengwa katika misingi ya rahma.

ELIMU NI NINI?

Elimu ni kuitambua haki kupitia dalili zake, na kinyume chake ni ujinga (kutoitambua haki kwa dalili)

Pamesemwa kwenye ubainifu wa mahusiano kati ya elimu na matendo. "Elimu huyasemeza matendo ikiwa yatakubali elimu itakaa (kwa mtu huyo) na ikiwa matendo yatagoma kuifata elimu basi elimu huondoka kwa ajili hiyo hakuna faida yoyote ya elimu isiyo na matendo, pale mwanafunzi anapojifunza inampasa aifanyie kazi elimu yake na kama hakufanya hivyo anakuwa sawa sawa na mayahudi wanayo elimu lakini hawaifanyii kazi. Amesema Allah "Wale tuliowapa kitabu wanayajua haya kama wanavyowajua watoto wao 2:147" Na watu wa mwanzo kabisa watakao chomwa moto ni wa aina tatu, miongoni mwao ni mjuzi aliyojifunza elimu lakini hakuifanyia kazi, Amesema mshairi "Na kila mjuzi ambaye hakufanyia kazi elimu yake, Ataadhibiwa kwanza kabla ya washirikina."

**KULINGANIA KUNA SHARTI NA KANUNI NI LAZIMA
UZIFUATE NA ZA MUHIMU KABISA NI HIZI ZIFUATAZO:**

3. Kuilingania
hiyo elimu. (Haki)

1. Iwe huko
kulingania ni
kwa ajili ya
kutafuta radhi
za Allah

2. Kulingania
huko kuwe
kumejengwa
katika misingi
ya elimu ya
kisheria

3. Da'wa iwe
kwa hekima
na subira

4. Kutimie
kuchunga hali
zote za wanao
linganiwa

DALILI YA SHARTI HIZI NI KAULI YAKE ALLAH (Subhanahu wataala)

Sema hii ndio njia yangu ninayolingania kwa **Allah** kwa ujuzi mimi na wanaonifuata, Na ametakasika **Allah** wala mimi si katika washirikina. 12: 109

SEMA HII NDIO NJIA YANGU Kinachokusudiwa hapa ni sharia aliyokuja nayo Mtume swalalahu walaih wasalam

NINALINGANIA KWA **ALLAH**..... Mwenye kulingania hasa kwa **Allah** ni Yule mwenye Ikhlasi ambayo lengo lake ni kuwafikisha watu kwa **Allah**.

KWA UJUZI..... (BASIRA) ni elimu na basira ya hapa inakusanya

Elimu ya sharia

Hali ya mlinganiwa

Njia yenye kufikia lengo

Bila shaka Mtunzi (Sheikh) Allah amrehemu anasema:

Utakaposima kisha ukaifanyia kazi elimu inakupasa upite kwenye njia ambayo aliyoipita Mtume **swalla llahu alayhi wasallama** na masahaba pamoja na waja wema waliotangulia, kwa sababu Allah amesema:-

“Sema hii ndio njia yangu ninayoilingania kwa **Allah**, kwa (kutumia) ujuzi mimi pamoja na wanaonifuata Kwa mujibu wa aya hii ni lazima kufanya da’wah


4. Kuvumilia maudhi katika mchakato wote wa kiutendaji.

Na dalili ya hoja hii ni kauli yake **Allah**.

“Naapa kwa zama

- (1) Hakika binadamu bila shaka yumo katika hasara.
- (2) Isipokuwa tu wale walioamini na wakatenda mema na wakausiana kwa haki na wakausiana kusubiri

1. Mwandishi (Sheikh) Allah amrehemu baada ya kuizungumzia da’awah na subira utadhani anakuambia haya: Hakika Yule ambaye anapita njia hii yatampata mambo mengi tu kama yalivyowapata mitume – Alayhimu-salammu kwa hali hii ni lazima mtu awe na subira.



**IMAMU IBNUL QAYYIM (ALLAH AMREHEMU) AMEIGAWA
SUBIRA KATIKA VIGAWANYO VITATU.**

1. Kufanya subira
katika kumtii
Allah ili
kuitekeleza twaa
(utiifu) ipasavyo

2. Kufanya subira
kutokumuasi
Allah ili
kujiepusha na
madhambi

3. Kufanya subira
juu ya qadari za
Allah zinazoleta
majonzi.

**2. BAADA YA MWANDISHI KUTAJA MAMBO MANNE YA MSINGI AKATAJA DALILI
ZAKE KUTOKA NDANI YA QUR'AN NAYO NI SURATUL-ASRI NA MARA ZOTE
MWANDISHI AMEKUWA AKITAJA MASAILI MBALIMBALI AKIAMBATANISHA NA
DALILI ZAKE. UNAJUA SABABU?**

1. Ili amlee
mwanafunzi
kufuata mambo
kwa dalili si kwa
taqlidi (kibubusa)

2. Ili mwanafunzi
awe na hoja
madhubuti
atakazozitumia
kumpinga kila
anayeenda
kinyume na dalili.

3. Ili mwanafunzi awe
na uwezo wa
kuzitohoa hukumu
kutoka kwenye
dalili zake juu ya
misingi maalum.

Amesema Imamu Shafii (Allah amrehemu) “Lau Allah asingeteremsha hoja yoyote kwa waja wake isipokuwa sura hii (suratul Asri) ingeliwatosheleza.”

Na amesema Imamu Bukhari (Allah amrehemu. *“Huu ni mlango wa kujifunza elimu kabla ya kusema na kutenda, na dalili juu ya hilo ni kauli yake Allah! Basi tambua ya kwamba hapana anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Allah na omba msamaha kwa dhambi zako na za waumini wanaume na waumini wanawake”*

Allah amrehemu Imamu Shafii makusudio yake ni kwamba Sura hii tu peke yake inatosha kusimamisha hoja kwa viumbe ili wajifunze watende walinganie na wafanye subira.

Ikiwa sura hii moja tu inajenga hoja hizo je kwa sura zingine zilizo bakia kwenye Qur'an hali ikoje? Basi Qur'an yote ni hoja.

Amiri Muuminina kwenye fani ya hadithi ameweka mlango kwenye kitabu chake SAHIHUL-BUKHAR. Akasema:

Huu ni mlango wa elimu kabla ya kusema na kutenda na akaitaja dalili

Hivyo kwanza kabisa ni wajibu kusoma kabla ya kusema na kutenda. Haifai mtu yeyote kutenda jambo bila ya ujuzi, na ikiwa mtu huyo atatenda bila ujuzi juu ya jambo hilo huyo atakuwa sawa sawa na wakristo.

JAMBO LA PILI

MAMBO MATATU YA MSINGI (KATIKA UISLAMU)

Tambua ewe mwanafunzi “Allah akurehemu” ni kwamba inampasa kila muislamu wa kike na wa kiume kujifunza mambo haya matatu na kuyafanyia kazi hapa katika mambo

Mwandishi ameanza kwenye hii sehemu ya kitabu hiki kwa kumuombea dua.

Amemuombea dua mwanafunzi kwenye kitabu hiki katika sehemu tatu.

Mwanzoni alipoanza kuelezea mambo manne ya msingi kisha matatu ya msingi, na sehemu ya tatu ni katika Tauhid iliyonyooka”

UTANGULIZI KABLA YA KUSHEREHESHA MAMBO MATATU:

TAUHID

Tauhid kwa mujibu wa lugha ya kiarabu ni neno lenye maana ya kukifanya kitu kuwa kimoja (Kukipwekesha).

Tauhid kisheria: Ni kumpwekesha Allah katika ibada zote zinazomuhusu yeye tu katika Rububiyya, Uluhiyya na majina na sifa zake.

TAUHID INAGAWANYIKA VIGAWANYO VITATU

AL-RUBUBIYYAH:

Nako ni kumpwekesha Allah kwenye matendo yake, kama vile kuhuisha, kufisha, kuruzuku, kuumba, kuendesha ulimwengu n.k

AL-ULUHIYYA:

Huku ni kumpwekesha Allah kwenye ibada zote tunazozitenda.

AL-ASMAI WAS-SIFATI:

Huko ni kumpwekesha Allah kwenye majina na sifa zake alizojisifia kwenye Qur'an au kwenye ulimi wa Mtume wake. Bila kubadilisha maana zake au kuzigeuza au kuzijengea taswira au mifano na viumbe

JAMBO LA KWANZA LA MSINGI:

Bila shaka Allah ndiye aliyetuumba na akaturuzuku wala hakutuacha bure bali alitutumia mtume kwa atakaye mtii mtume huyo ataingia peponi na atakae muasi ataingia motoni. Na dalili yake ni kauli ya Allah (**Hakika sisi tumemtuma kwenu mtume aliyeshahidi juu yenu kama tulivyomtuma mtume kwa Firauni lakini Firauni alimuasi mtume huyo basi tukamshika mshiko wa mateso (AL-MUZAMIR) (16:17)**)

MAJINA YA ALLAH NA SIFA ZAKE YANA MIPAKA HUCHUNGWA MAANA ZAKE KWA MUJIBU YALIVYOKUJA KWENYE QUR'AN NA SUNNA.

- Nako ni kuthibitisha majina na sifa ambazo Allah ameithibitishia nafsi yake au alimthibitishia mtume wake.
- Kukanusha majina na sifa ambazo Allah amezikanusha juu yake au amemkanushia mtume wake **swalla llahu alayhi wasallama** kama vile kusahau, kusinzia, kuchoka n.k. Inapasa kuamini haya bila ya kubadilisha maana ya majina na sifa zake, au kuzigeuza au kuzijengea taswira na kuzifanyia mifano kwenye viumbe.

UFUPISHO WA MAMBO MATATU YA MSINGI

JAMBO LA KWANZA.

Ni kumpwekesha Allah kwenye matendo yake na majina na sifa zake tukufu

JAMBO LA PILI.

Kumpwekesha Allah kwenye Ibada.

JAMBO LA TATU.

Ni kujitenga mbali kabisa na kila shiriki pamoja na washirikina.

Katika jambo la kwanza mwandishi Allah amrehemu amethibitisha ndani yake kumpwekesha Allah katika matendo yake na pia katika majina na sifa zake. Ya kuwa Allah pekee ndio Muumba mtoaji wa riziki na hakutuacha bure bali alitutumia Mtume ili kutufundisha maamrisha na makatazo

**LENGO KUU LA ALLAH SUBHANAHU WATAALA
KUTUMA MITUME (AMANI ZIWE JUU YAO)**

Kuwasimamishia hoja viumbe wake. Allah subhanahu wataala amesema: "Sisi hatuadhibu mpaka tumpeleke mtume." 17:16

Kuwarehemu viumbe wake. "Nasi hatukukutuma ila uwe ni rehome kwa walimwengu wote". 21:108.

JAMBO KUU LA PILI NDANI YAKE KUNA KUTHIBITISHA HAKI YA KUABUDIWA KWA ALLAH MTUKUFU.

2. Hakika Allah haridhii kushirikishwa na yeyote kwenye ibada zake, si kwa malaika wala mtume yeyote.

Na dalili ju ya hilo Allah amesema:

Na hakika misikiti ni ya Allah, Basi msimuabudu yeyote pamoja na Allah (72:19)

Amesema mwandishi Allah amrehemu. Hakika Allah haridhii kushirikishwa pamoja naye yeyote, si mtume, walii, jinni, malaika, mja mwema au mwingine yeyote hata aweje!

KATIKA NENO MASAJIDI KUNA KAULI TATU AMBAZO INAFAA

1 Misikiti iliyojengwa kwa lengo la
kuabudiwa Allah peke yake ndani ya misikiti hiyo

2 (Masajidi)
Linachukua maana ya viungo vyote vya kusujudia.

3 ARDHI: Amesema mtume swalalahu walaih wasalam na Ardhi imefanywa kwangu kuwa ni msikiti na sehemu ya kujitaharishia

JAMBO KUU LA TATU.


Hakika yeyote atakae mtii mtume ***swalla llahu alayhi wasallama*** na akampwekesha Allah subhanahu wataala Haifai kabisa kwa mtu huyo kuwafanya kuwa marafiki wale wote wenye kumpiga vita Allah na mtume wake hata kama atakuwa ni ndugu yake wa karibu mno.

Dalili yake Allah anasema: “Huwakuti watu walio muamini Allah na siku ya mwisho wanawapenda wanao mpinga Allah na mtume wake, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao au jamaa zao.

Hao ameandika katika nyoyo zao Imani, na amewapa nguvu kwa roho itokayo kwake: Na atawaingiza katika mabustani yapitayo mito kati yake humo watakaa milele, Allah awe radhi nao na wao wawe radhi naye.

Hao ndio Hizbullah kundi la Allah. Hakika kundi la Allah ndilo lenye kufanikiwa. (58:22)

KWENYE JAMBO KUU LA TATU MWANDISHI AMEBAINISHA WAJIBU WA KUJITENGA MBALI NA SHIRKI NA WASHIRIKINA.



1. KWA MOYO:

Ni kuwachukia makafiri na sikukuu zao na sherehe zao na hasa zinazoambatana na mambo ya shirki na bidaa mbalimbali walizo nazo.

2. KWA ULIMI:

Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayoyaabudu (43:26)

Sema: Enyi makafiri (1) Siabudu mnacho kiabudu (2) Wala nyinyi hamuabudu ninaye muabudu (3) Wala sitaabudu mnacho abudu (4) Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu (5) Nyinyi mna dini yenu na mimi nina dini yangu (6) (109:1-6)

3. KWA VIUNGO:

Ni kutoshirikiana nao kwenye sherehe zao au kucheza nao au kuvaa kama wao, au kufuata itikadi yeyote waliyonayo.

JAMBO LA TATU

UMUHIMU WA KUJIFUNZA TAUHID

Tambua ewe mwanafunzi! Allah akuongoze: Hakika Tauhid iliyonyooka ni mila ya Nabii Ibrahim.

Nako ni kumuabudu Allah pekee na kumtakasia dini yake, na kwa ajili hiyo ndio Allah amewaamrisha watu wote na amewaumba kwa ajili hiyo tu. Kama alivyosema:

Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi. (51:57)

Na maana ya waniabudu hapa wanipwekesha (kwenye ibada zangu).

Na amri kuu aliyoiamrisha Allah ni Tauhid. Nako ni kumpwekesha Allah kwenye ibada. Na katazo kuu alilolikataza ni shirki nako ni kumchanganyia Mungu mwingine katika kumuabudu Allah.

TAUHID ILIYONYOOKA

Kilugha imetoholewa katika neno hanafi lenye maana ya kuegemea upande.

Ama kisheria:

Hiyo ni mila iliyoacha upande wa shirki na imeelekea upande wa Ikhlas, Tauhid na Imani

Nyenyekevu kwa Allah mwongofu) (16:120)

Kwa maana amemwelekea Allah na ameipa mgongo shirki.

Muongofu ni Yule anaeifuata Tauhid muda wote na anajitenga mbali na shirki

Hapa mwandishi ameweka wazi sababu kwanini tujifunze Tawhid. Na tumeishataja umuhimu wa kujifunza hapo nyuma

UTAMBULISHO WA TAUHID KAMA TULIVYOUTAJA KWENYE UTANGULIZI

Tauhid kilugha inatokana na asili ya neno (wahhada) pale mtu anapokifanya kitu kinakuwa pweke.

Tauhid kisheria ni kumpwekesha Allah na vyote vinavyo muhusu kwenye kila Tauhid Rububiyya, Uluhiyya na Tauhid ya majina na sifa zake tukufu

Amesema mtunzi wa kitabu na maana ya neno “waniabudu” ni wanipwekesha. Na maana hii ndio kauli ya Ibn Abbasi Allah amridhie pale aliposema: Hakika kila neno Ibada ndani ya Qur’an lina maana ya Tawhid (upwekeshaji). Katika aya hii “Na mwabuduni Mola wenu Mlezi” maana yake ni Mpwekesheni Mola wenu..... Na maana ya aya hii: Enyi watu muabuduni Mola wenu Mlezi.... (Mpwekesheni).

JAMBO LA NNE

MISINGI MITATU (YA IMANI):

Utakapoambiwa! Ni ipi misingi mitatu ambayo ni lazima kwa kila mtu aitambue?

Basi wewe sema: Ni kumjua Allah, Dini yake na Mtume wake Muhammad (*swalla llahu alayhi wasallam*)

Mtunzi Allah amrehemu ameanza kwa kuitaja misingi mitatu ambayo ndio maswali matatu ya kaburini.

Na akaamsha umakini wa msomaji au atakae sikia swali hilo na kisha akalijibu swali hilo mwenyewe

Pale utapoambiwa: Ni nani Mola wako mlezi? Basi useme: Allah ndio Mola wangu mlezi ambaye ndio aliyeniumba akanilea na kuwalea watu wote (viumbe wote) kwa neema zake, na yeye tu ndio ninaye muabudu sina ninaye muabudu zaidi yake. Na dalili juu ya hilo ni kauli yake Allah subhanahu wataala Sifa zote njema zinamstahiki. Allah Mola mlezi wa viumbe wote. Na ukimtoa Allah subhanahu wataala vilivyosalia vyote ni viumbe vyake na mimi ni miongoni mwa viumbe hao.

Kwa hapa mtunzi anaweka bayana msingi wa kwanza, akabainisha ya kuwa Mola mlezi anayestahiki kuabudiwa ni Allah pekee na akaitaja dalili yake ni kauli ya Allah subhanahu wataala Sifa zote njema zinamstahiki Allah Mola mlezi wa viumbe wote”

Ne “Rabbu” maana yake ni muabudiwa. Na aya hii imebeba maana zote tatu za aina za Tauhid.

AL-HAMDU:

Ndani yake kuna ithibati za Tauhid ya majina na sifa (za Allah).

LILLAHI:

Ndani yake kuna ithibati ya Tauhid ya Ibada (Uluhiyya)

RABBI:

Ndani yake kuna ithibati ya Tauhid ya utendaji wa Allah subhanahu wataala

Ukimtoa Allah subhanahu wataala vyote vilivyosalia ni viumbe, na mimi nikiwa ni kiumbe basi ni lazima itoe shukrani za dhati kwa Muumba mwenye kuneemesha na mwenye hisani subhanahu wataala

Ikiwa utaambiwa: Kwa dalili zipi umeweza kumjua Mola wako mlezi?

Basi wewe utasema: Nimemjua Mola wangu kupitia ishara zake na viumbe vyake, na miongoni mwa ishara zake ni usiku na Mchana, Jua na Mwezi na miongoni mwa viumbe vyake ni Mbingu saba na Ardhi saba na viumbe vyote vilivyomo ndani yake na viumbe vyote vilivyomo kati ya Mbingu na Ardhi.

DALILI ZAKE NI KAULI YAKE ALLAH

“Na katika ishara zake ni usiku na mchana na jua na mwezi. Basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Allah aliye viumba, ikiwa nyinyi mnamuabudu yeye tu. (41: 37).

NA KAULI YAKE ALLAH SUBHANAHU WATAALA

Hakika Mola mlezi wenu ni Allah aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha akatawala juu ya kiti cha enzi. Huufunika usiku upesiupesi. Na jua, na mwezi,

Mwandishi ameanza kutaja mkusanyiko wa ishara za maumbile na viumbe ambavyo vinafahamisha uwepo wa Allah, na ndizo zinazothibitisha ya kuwa, hakuna Mola mlezi muabudiwa yeyote anayestahiki kuabudiwa isipokuwa ni Allah, na akaleta dalili juu ya haya kutoka ndani ya Qur’ani kama zilivyotajwa kwenye matini ya kitabu.

Kila kiumbe kilichopo ni alama tosha ya kuwepo Allah subhanahu wataala

Lakini Imam ametofautisha kati ya ishara na kiumbe, kwa sababu ishara inabadilika kama vile mchana na usiku.

Na chochote kinachobadilika kinakuwa ni dalili yenye nguvu kushinda kila ambacho hakibadiliki.

Katika aya hii ya 21 iliyopo kwenye suratul-Baqarah, wamesema baadhi ya wanachuoni: Hakika aya hii ndani yake ndio kuna wito wa kwanza ndani ya Qur’an (Enyi watu).

Na nyota zinazotumika kwa amri yake.
Fahamuni! Kuumba na amri ni zake.
Ametukuka kabisa Allah, Mola mlezi wa
viumbe vyote. (7:54) 1

NA MAANA YA RABBU NI MWABUDIWA, NA DALILI YAKE NI:-

Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi
aliyekuumbeni nyinyi na wale wa kabla
yenu ili mpate kuokoka (21)

(Allah) ambaye amekufanyiaeni hii ardhi
kuwa tandiko, na mbingu kama paa, na
akateremsha maji kutoka mbinguni na
kwayo akatoa matunda yawe riziki zenu:
Basi msifanyie Allah washirika na hali nyinyi
mnajua (22)

Ibn Kathir Allah amrehemu amesema: Yule
aliye viumba vitu vyote hivi huyo ndio
anayestahiki kuabudiwa.

Na aina za ibada ambazo Allah subhanahu
wataala ameziamrisha ni kama vile Uislamu,
Imani na Ihsani, na miongoni mwa ibada ni
kuomba, khofu, kutaraji,

Na ndani ya aya hiyo ndiyo kuna kitendo cha
kwanza cha kuamrisha ndani ya Qur'an
(Abuduni) Pwekesheni.

Na ndani yake ndio kuna katazo la kwanza
ndani ya Qura'n, (Basi msimfanyie Allah
washirika na hali nyinyi mnajua). Hilo ni
katazo la shiriki.

3- Yule aliye pekee kwenye Tauhid ya
matendo ndio anayepaswa kupwekeshwa
kwenye Tawhid ya ibada.

Mtunzi ameifatisha kauli ya Ibn Kathiri kwa
kutaja idadi ya ibada za moyoni na za
kiwiliwili pamoja na kuweka dalili kutoka
kwenye Qur'an ya kila amali kwa mpangilio
ufuatayo:-

MAOMBI HUGAWIKA KAMA IFUATAVYO:-

DUA YA IBADA.

Hiyo ni kila ombi
linalofanywa
kimatendo kama
kuswali,
kufunga, kuhiji,

DUA YA HAJA.

Hilo ni kila ombi
linalo ombwa kwa
maneno tu. Kama
kusema: nisamehe,
nirehemu

Kumtegemea, kumpenda, kuwa na khofu, kunyenyekea, kuogopa, kurejea, kuomba msaada, kuomba ulinzi, kuomba ukovu, kuchinja, kuweka nadhiri, na mengineyo miongoni mwa aina mbalimbali za ibada alizoziamrisha Allah. Ibada zote hizo zinamstahiki Allah peke yake na dalili yake ni kauli yake Allah subhanahu wataala

(Na hakika misikiti yote ni yake Allah basi msimuabudu yeyote pamoja na Allah)

Yeyote atakaye ipeleka ibada yoyote katika hizo kwa asiye kuwa Allah subhanahu wataala basi atakuwa ni mushiriki kafiri, na dalili juu ya hilo kauli yake Allah:

(Na anayemuomba pamoja na Allah Mungu mwingine hana ushahidi wa hili, basi bila shaka hisabu yake iko kwa Mola wake mlezi. Kwa hakika makafiri hawatafanikiwa. (23:117).

Kuyapeleka maombi hayo ya kimatendo kwa asiyekuwa Allah subhanahu wataala hiyo ni shirki kubwa

Hukumu ya maombi ya maneno ndani yake kuna ufafanuzi, nayo inagawanyika vigawanyo viwili kama ifuatavyo:-

DUA YA HAJA (MAHITAJI) INAGAWANYIKA SEHEMU KUU MBILI

kwenye mambo ambayo hakuna mwenye uwezo nayo isipokuwa Allah subhanahu wataala pekee kuyapeleka maombi hayo kwa mwingine. Hiyo ni shirki kubwa.

Kwenye mambo ambayo yamo ndani ya uwezo wa binadamu itafaa ila kwa kufuata masharti yafuatayo:

MASHARTI YA MAOMBI YA HAJA

1- Yule anayeombwa ni lazima awe hai, kufuatana na sharti hili linamtoa maiti haitofaa kumuomba.

2- Yule anayeombwa awepo, (Mbele ya muombaji) Kwa sharti hili linamtoa asiyekuwepo, aliyembali na muombaji

Na imekuja katika hadithi

“Dua ndio ubongo wa kila ibada”

Na dalili ni kauli ya Allah subhanahu wataala

Na Mola wenu mlezi amesema niombeni nitakuitikieni, kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu mimi wataingia Jahannamu wadhalilike. (40:60)

3- Yule mwenye kuombwa ni lazima awe na uwezo wa kulitenda ombi hilo. Kwa sharti hili linamtoa kila asiye na uwezo wa kulifanya ombi hilo

4- Muombaji aitakidi ya kuwa Yule muombwaji yeye ni sababu tu katika kutenda siyo ndio mwezeshaji kwa dhati yake.

Ama muombaji akiitakidi ya kuwa huyu anayeombwa ana uendeshaji wa siri (Uliofichikana) wa huu ulimwengu, tena ana uwezo wa kuleta manufaa na kuondoa madhara (mabalaa). Hii itakuwa ni shirki kubwa.

NB: Sisi tunajifunza hukumu ya matendo tu, ama hukumu ya mtendaji inahitajia kumsimamishia hoja (dalili) na kusiwepo pia shubha.

Na wanachuoni wao ndio wanaostahiki kutoa hukumu ya mtendaji kuwa yeye ni muumini (kwa kutenda jambo Fulani) au ni kafiri.

**WAMEGAWANYIKA WATU KWENYE KUITAKIDI KWENYE
SABABU KATIKA VIGAWANYO VITATU.**

Kigawanyo cha kwanza.

Wanaitakidi, na wanajaalia yale aliyoyajaalia **Allah Subhanahu Wataala** kuwa ni sababu sababu. Na hii ndio sahihi

Kigawanyo cha pili.

Wanaitakidi na wanajaalia yote ambayo hakuyajaalia **Allah Subhanahu Wataala** kuwa ni sababu sababu. Na hii ni shirki ndogo

Kigawanyo cha tatu.

Wanaitakidi ya kwamba hakika sababu yenyewe kwa dhati yake ina athiri na kwa kupitia hiyo sababu inaleta manufaa na inaondoasha madhara. Basi hii ndio shirki kubwa.

Sababu za kisheria

Ni kama vile kufanya Rukiya ya kisheria hakika amejaaalia **Allah Subhanahu Wataala** Ruqya ya kisheria kuwa ni sababu ya kuondoa

Sababu za hisia

Ni kama vile kutumia dawa kwa hakika amejaaalia **Allah** dawa kuwa ni sababu ya kujitibu

Hadithi: (dua ni ubongo wa ibada) Hadithi hii ni dhaifu na ilio sahihi ni kauli ya Mtume *swalla llahu alayhi wasallama* (Dua ndio ibada)

Vipi dua iwe ni ibada?

Aya ndio inayojulisha hivyo: (Na Mola wenu mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni, kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu mimi wataingia Jahannamu wadhalilike.) Amesema **Allah Subhanahu Wataala** (kuniabudu mimi) kwa hiyo hii ni Dalili ya kwamba dua ni ibada.

(1) Khofu: Nayo ni athari inayopatikana kwa kuchelea jambo ambalo ndani yake kuna maangamizi, au kuna madhara, au kuna maudhi. Na Allah Subhanahu Wataala amekataza kuwakhofia viongozi wa masheitani. Na akaamrisha kumkhofia yeye

Na dalili ya khofu ni kauli yake Allah Subhanahu Wataala (Basi msiwaogope bali niogopeni mimi mkiwa nyinyi ni waumini)(1)

Na dalili ya kutaraji ni kauli yake Allah Subhana Wataala (Mwenye kuraraji kukutana na mola wake mlezi basi na atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya mola wake mlezi.) (2)

KHOFU ZIPO AINA TATU

Khofu ya Ibada na kuadhinisha, na ya siri: Nayo ni kumkhofia mwenye kuabudu yule anayeabudu, ndani yake kuna kujidhalilisha na kunyenyekea, na kumtukuza muabudiwa. Khofu ya namna hii ni wajibu kwa Allah, na kuielekeza kwa mwingine asiekua Allah ni shirki kubwa.

Khofu ya kimaumbile. Nayo ni kama vile mwanadamu anapo muogopa simba, moto, adui au mnyama anaeshambulia.... Khofu ya namna hii ni halali.

Khofu iliyoharamishwa. Ni kama vile kukata tamaa katika rehema za Allah. Au kumtii kiumbe katika kumuasi muumba.

(2) Kutarajia.

Kutarajia ni kutamani ya mwanadamu kwa jambo lililokua karibu kupatikana. Na mda mwingine huwa linakua mbali kupatikana lakini hulishusha kama vile lipo karibu

kupatikana. Matarajio ambayo ndani yake kuna kujidhalilisha na kunyenyekea hayatakiwi kuwepo kwa mtu isipokua kwa ajili ya Allah Subhanahu Wataala.

Na kuyaelekeza matarajio ya namna hiyo kwa asiekua Allah Subhanahu Wataala jambo hilo ni shirki kubwa.

Hivyo matarajio yenye kushukuriwa na kupendwa yanakuwa kwa Yule atakae mtii Allah. Na akatarajia thawabu, au akatubia kwa maasi yake, na akataraji kukubaliwa toba yake.

Ama kutarajia bila kufanya matendo mema huko ni kujidanganya pia ni matarajio yasio kubalika na kupendeka.

DALILI YA KUMTEGEMEA ALLAH

Ni kauli yake Anasema: (Na mtegemeeni Allah ikiwa nyinyi ni waumini)

Na kauli yake (Anaemtegemea Allah yeye humtosha) (1)

Dalili ya Raghba na Rahba na Khushui ni kauli yake mtukufu (Hakika wao walikuwa wepesi wakutenda mema, na wakituomba kwa shauku na khofu. Nao walikuwa wakitunyenyekea) (2)

UTAMBULISHO WA TAWAKKULI

Tawakkuli kilungha ni kukitegemea kitu.

Tawakkuli kisheria ni kumtegemea Allah kiukweli na kumuamini yeye na kuchukua sababu za kisheria.

Hapana budi katika Tawakkuli yapatikane mambo matatu

Ukweli katika kumtegemea Allah

Kuamini kwamba Allah Subhanahu Wataala ni mwenye kutekeleza yote alioahidi

Kufanya sababu za kisheria.

(2) Raghba: Ni kupenda kukifikia kitu chenye kupendwa. Rahba: ni khofu yenye kusababisha kukikimbia kinacho khofiwa. Kwahiyo Rahba ni khofu yenye kukutana na matendo mema.

Khushui: ni kunyenyekea utukufu wa Allah, kwa namna ya mtu kujisalimisha kwa Allah katika aliohukumu kiulimwengu na kisheria. Yeyote ambae ana muendea Allah Subhana Wataala, hapana budi awe na khofu pamoja na matarajio. Vyote viwe sawa, usizidi upande wowote katika hivyo. Ukizidi upande mmoja wapo ataangamia. Hivyo lazima iwe khofu na matarajio kama vile mbawa mbili za ndege.

- 1) **KHASHYAH** : Ni khofu iliyojengeka kutokana na elimu aliyokuanayo mtu. Kwakumtukuza Yule anaemukhofia. Na kwa ukamilifu wa nguvu zake.
- 2) **INAABABAH**: Ni kumrejea Allah mtukufu kwa kumtii na kujiepusha na maasi. Allah anasema: (Na rejeeni kwa Mola wenu mlezi, na silimuni kwake) kwa maana salimisha jambo lako kwa Allah Subhana Wataala, kwani wewe ni mtumwa wake, na mtumwa hapana budi ajisalimishe kwa Bwana wake, na bwana mwenyewe ndie Allah. Kama alivyosema mtume rehma na amani ziwe juu yake. (Bwana ni Allah).
- 3) **ISTIANAH**: Ni kuomba msaada. Allah anasema(wewe tu tunakuabudu, na wewe tu tunakuomba msaada) katika aya hii kimetangulizwa kitu ambacho haki yake kichelewe. Hii inajulisha (Hasri,) kwa maana hakuna tunae muabudu wala kumuomba msaada isipokua ni wewe tu.
- 4) **ISTIADHAH**: Ni kuomba ulinzi na kinga kwa Allah kutokana na yenye kuchukiza.
- 5) **ISIGHAATHAH** : Ni kuomba kuokolewa kutokana na matatizo na maangamizi. Kuomba msaada na kutaka ulinzi, na kutaka kuombewa hivi vyote unaruhusiwa, kumuomba kiumbe katika vile alivyoweza kukusaidia kwa masharti manne: Huyo kiumbe awe hai, awepo hapo mahala awe ana uwezo wa kufanya hicho anachoombwa, awe ni sababu
- 6) **Kuchinja**: Ni kuitoa roho, kwa kumwaga damu kwa namna maalum.

- 1) **Dalili ya kumkhofu Allah ni kauli yake** Allah mtukufu: (Basi msiwaogope wao lakini niogopeni mimi)
- 2) **Dalili ya kumrejea Allah ni kauli yake** (Na rejeeni kwa Mola wenu mlezi na silimuni kwake)
- 3) **Dalili ya kuomba msaada ni kauli yake Allah.** (Wewe tu tunakuabudu na wewe tu tunakuomba msaada) Na katika Hadithi (Utakapotaka msaada basi muombe msaada Allah)
- 4) **Dalili ya kuomba ulinzi ni kauli yake Allah** (Sema najikinga kwa Mola mlezi wa mapambazuko) (Sema: Najikinga kwa Mola mlezi wa Wanadamu)
- 5) **Dalili ya kuomba kuokolewa ni kauli yake Allah:** (Mlipokuwa mkimuomba msaada Mola wenu mlezi, naye akakujibuni)
- 6) **Dalili ya kuchinja ni kauli ya Allah.** (Sema: hakika sala yangu na Ibada zangu na uhai wangu ni kwaajili ya Allah Mola mlezi wa viumbe vyote. Hana mshirika) Na katika Hadithi (Allah amelaani mwenye kuchinja si kwa ajili ya Allah)

KUCHINJA KUMEGAWANYIKA SEHEMU TATU

Dalili ya nadhiri ni kauli yake Allah mtukufu.

(Wanatimiza ahadi (Nadhiri) na wanaiogopa siku ambayo shari yake inaenea sana)

Kuchinja kwa ajili ya Allah. Kama vile wanyama wa zawadi, na waudh-hiya – na sadaka mbalimbali

Kuchinja sio kwa ajili ya Allah. Kwa kupenda na kutukuzu. Kama vile kumchinja jinni. Na watu wa makaburini. Na hii ni shirki kubwa

Kuchinja kuliko halalishwa. Kama vile mbuzi wa nyama na kumkirimu mgeni na kwa ajili ya biashara

UTAMBULISHO WA NADHIRI

Kilugha: ni kuahidi na kujilazimisha

Kisheria: ni mtu kuilazimisha nafsi yake kitu ambacho sio wajibu

❖ **Tanbihi:** Kuna ziada ya ufafanuzi katika masuala ya kuchinja itakuja ziada hiyo katika kitabu cha Tauhidi kwa idhini ya **Allah**.

❖ **Tanbihi:** Nadhiri ina vigawanyo na masharti na kafara utakuja ufafanuzi wake katika kitabu cha Tauhidi kwa idhini ya **Allah**.

AINA ZA NADHIRI

Kuweka nadhiri kwa ajili ya Allah

Kuweka nadhiri sio kwa ajili ya Allah


❖ Mtunzi wa kitabu hiki amezitaja hizi ibada sio kwa malengo ya kuzidhibiti. Bali ni kwa njia ya kupiga mifano tu. Kwani kuna ibada nyingi tu lakini hazikutajwa hapa. Ushahidi ni kwamba yeyote atakae elekeza au kuzitumia Ibada hizi au zingine sio kwa ajili ya Allah basi atakuwa amefanya shirki.

1. Ameingia mtunzi katika kuelezea msingi wa pili nao ni kuitambua mja dini yake na akaanza kuutambulisha Uislamu Akasema:

Uislamu ni kujisalimisha kwa **Allah** kwa kumpwekesha na kumnyenyekea kwa kumtii na kujiepusha na shirki na washirikina

Huu ndio utambulisho wa uislamu ni kusalimisha mambo yako kwa **Allah** Subhanahu Wataala kwa sababu wewe ni mtumwa, na mtumwa ni lazima ajisalimishe kwa bwana wake. Na bwana ni **Allah**, kama alivyo sema mtume *swalla llahu alayhi wasallama*.

Kisha kaigawa Dini katika daraja tatu



2. Nguzo za uislamu ni tano ya kwanza ni;
Shahaada

Msingi wa pili.

Kuitambua dini ya uislamu kwa dalili. Uislamu ni kujisalimisha kwa **Allah**, kwa kumpwekesha na kumnyenyekea na kujiepusha na shirki na washirikina.

Uislamu una daraja tatu.

1. *Uislamu*
2. *Imaani*
3. *Ihsani*

Na kila daraja ina nguzo zake .

Daraja ya kwanza ni Uislamu.

Nguzo zake ni tano


1. Kushuhudia kwamba hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa ni **Allah** tu.
2. Na kushuhudia kwamba Muhammad ni mtume wa **Allah**
3. Kusimamisha swala
4. Kutoa zaka
5. Kufunga Ramadhani na kuhiji nyumba ya **Allah** tukufu.

Dalili ya shahada ni kauli yake Allah mtukufu: (Allah na malaika, na wenye elimu wameshuhudia kuwa hakika hapana Mungu ila yeye ndiye mwenye kusimamisha uadilifu: Hapana Mungu ila yeye mwenye nguvu na hekima)

Maana yake ni kwamba:

Hapana mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah (laailaaha) inakanusha vyote vinavyo abudiwa kinyume na Allah. (illa Allah) inathibitisha ibada kwa Allah pekee hana mshirika katika ibada zake kama ilivyo pia hana mshirika katika ufalme wake. Na tafsir inayo weka wazi maneno haya ni kauli yake Allah (Na pale Ibrahim alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayo yaabudu. Isipokuwa Yule aliyeniumba, kwani yeye ataniongoza. Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake ili warejee)

Ametaja mtunzi Allah amrehemu dalili ya shahada. Na akabainisha maana yake ambayo ni: Hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah.



Kukanusha ni kusema: (Hapana anaestahiki kuabudiwa)

Kuthibitisha ni kusema: (Isipokuwa Allah)

Mfumo wa maneno namna hii huleta husisho na thibitisho. Kwa maana ya kuhusisha na kuthibitisha ibada kwa Allah pekee, na kukanusha kwa mwengine. Ndio akasema mtunzi Allah amrehemu katika tafsiri ya maneno ya Allah akifafanua hilo: (Na pale Ibrahim alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi najitenga mbali na hayo mnayo yaabudu. Isipokuwa Yule aliye niumba, kwani yeye ataniongoza.

❖ Lau atasema msemaji:

Maana ya (Shahadatu anlaa ilaaha illa allahu) Hapana muabudiwa isipokuwa Allah?

Tutamwambia, haya maneno ni batili.

Kwani kwa maneno hayo yana sahihisha kila kinachoabudiwa kinyume na Allah. Lakini pale anaposema na kuongeza neno (kwa haki) akasema (Hapana Mola muabudiwa kwa haki isipokuwa Allah) hii itakuwa ni dalili kwamba yeye ana pinga vyote vinavyo abudiwa kinyume na Allah. Na ni kwamba Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah.

Na kauli yake Alla anasema:

Sema: Enyi watu wa kitabu njooni kwenye neno lililo sawa baina yetu na nyinyi, ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Allah, wala tusimshirikishe na chochote, wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa waola walezi badala ya Allah. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.(1)

❖ Lau atasema msemaji:

Maana ya (laa ilaaha illa allah) ni hapana Mola mlezi wa haki isipokuwa Allah?

Tutamwambia: haya maneno ni sahihi. Lakini sio tafsiri ya (Laa ilaaha illa allah). Hii ni Tauhid Rububiyya (matendo ya Allah) kwani Tauhid hii waliikubali makafiri ambao alipelekwa kwao mtume Muhammadi, **swalla llahu alayhi wasallama**. Na haikuwaingiza katika uislamu.

(1)(Sema: Enyi watu wa kitabu! Njooni kwenye neno lililo sawa baina yetu na nyinyi) Aya hii ndani yake kuna ushahidi wa kubatilisha ukaribu baina ya dini.

Na dalili ya kushuhudia ya kwamba Muhammadi ni mtume wa Allah, ni kauli yake Allah anasema: (Hakika amekwisha kujieni mtume kutokana na nyinyi wenyewe, yanamuhuzunisha yanayo kutaabisheni. Ana kuhangaikieni sana. Kwa waumini ni mpole na mwenye huruma)(1)

Maana ya kushudia kwamba Muhammadi ni mtume wa Allah: Ni kumtii katika aliloamrisha, na kumkubali katika alioeleza. Na kujiepusha na yale alio kataza na kukemea. Na asiabudiwe Allah isipokuwa kwa namna aliofundisha yeye (2)

- (1) Ameitaja mtunzi aya hii Allah amrehemu, ikiwa ni dalili katika kushuhudia kwamba Muhammadi Swalla allahu alayhi wasallam ni mtume wa Allah. Pia Allah ametia mkazo katika hiyo aya ya kushuhudia kwa vitu vitatu (kiapo kilicho kadiriwa,) (Laam) na (Qad).
- (2) Amebainisha mtunzi Allah amrehemu maana ya kushuhudia ya kwamba Muhammadi ni mtume wa Allah na hakika ina muwajibikia kila muislamu kuthibitisha hii shahada, kumtii mtume swalla allahu alayhi wasallam. Katika yote alioamrisha. Na kumkubali katika alioeleza, na kujiepusha na yote aliokataza na kuyakemea, na asiabudiwe Allah isipokuwa kwa namna aliofundisha na kubainisha. Rehma na amani zimfikie.

Hujulisha shahada ya kuwa Muhammadi ni mtume wa Allah. (ya kwamba yeye ni mja wa Allah asiabudiwe, pia ni mtume asipingwe) hii ikimaanisha kwamba:

Tumtii katika kila alichokamrisha. Rehma na amani zimfikie. Kwani yeye ni mfikishaji kutoka kwa Allah

Tumkubali katika alioeleza, Rehma na amani zimfikie, kwani yeye ni mkweli mwenye kukubaliwa. Rehma na amani zimfikie.

Tujiepushe na alichokataza na kukemea, kwa kukiweka alichokataza mtume Rehma na amani zimfikie katika upande mwingine na wewe uwe upande mwingine

Tusimuabudi Allah isipokuwa kwa maelezo au mafundisho aliokuja nayo mtume Rehma na amani zimfikie. Katika maelezo haya ndani yake kuna kuwa rudi wazushi katika dini

(1) Nguzo ya pili ni swala:

Nayo ni kumuabudu Allah, kwa vitendo na maneno maalumu. Huanzwa kwa Takbira na huisha kwa salamu. Na ndio jengo au nguzo ya dini. Na ilifaradhishwa kutoka kwa Allah moja kwa moja kwa mtume wake rehma na amani zimfikie, pale alipo pandishwa mbinguni rehma na amani zimfikie.

Nguzo ya tatu ni zaka.

Kilugha ni: kukua na kutwaharisha. Zaka zipo aina mbili: zaka ya mwili na zaka ya mali.

(2) Nguzo ya nne ni kufunga.

Kilugha ni kujizuwia kisheria

Ni kumuabudu Allah kwa kujizuwia na vyenye kufunguza, pamoja na kunuwia tokea kuchomoza kwa alfajiri mpaka kuzama kwa jua. Na funga ni katika aina bora za ibada, kwa kukusanya kwake aina tatu za subira. Na kutokana na ukubwa wa hadhi yake. Hakika Allah subhanahu wataala amenasibisha malipo ya funga kwake yeye mwenyewe.

(3) Nguzo ya tano ni Hija.

Hija kilugha ni kukusudia na kisheria ni kumuabudu Allah, kwa kutekeleza ibada kwa mujibu wa mafundisho yaliyo kuja katika sunna za mtume rehma na amani zimfikie. Kuhiji ni lazima kwa kila muislamu katika umri wake ni mara moja.

(1) Dalili ya swala na zaka ni kauli ya Allah mtukufu: *(Nao hawakuamrisha kitu ila wamuabudu Allah. Kwa kumtakasia dini, wawe waongofu, na washike sala, na watoe zaka. Ni hiyo ndiyo Dini madhubuti)*

(2) Na dalili ya swaumu, funga, ni kauli yake Allah: *(Enyi mlio amini mmeandikiwa saumu, kama walivyo andikiwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu)*

(3) Dalili ya Hija ni kauli ya Allah: *(Na kwa ajili ya Allah imewajibika watu wahiji kwenye nyumba hiyo kwa Yule awezae njia ya kwendea. Na atakae kanusha basi Allah si mhitaji kwa walimwengu.)*

Daraja ya pili ni Imani:

Na Imani ipo zaidi ya matawi sabini na tisa, imani ya juu zaidi ni kusema (*Laa ilaaha illa allah*) na ya chini yake ni kuondoa uchafu njiani. Na kuwa na haya ni sehemu katika imani. Na nguzo zake ni sita:

1. Kumuamini Allah
2. Kuamini malaika wake
3. Kuamini vitabu vyake
4. Kuamini mitume wake
5. Kuamini siku ya mwisho
6. Kuamini Qadari yake. (mipango)

Dalili ya hizi nguzo sita za Imani ni kauli yake Allah. (Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anayemuamini Allah na siku ya mwisho, na malaika na kitabu na manabii)

Dalili ya kuamini Qadari kauli yake Allah mtukufu (kwa hakika sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo (Qadari)

Daraja ya pili ni Imani

Imani kilugha ni kukiri na kisheria ni kukiri kwa ulimi, na kuitakidi kwa moyo na ulimi na kuitakidi kwa moyo na kutenda kwa viungo na moyo inazidi kwa kutii na inapungua kwa kufanya maasi.

Kwa hiyo imani kisheria lazima ikusanye hayo mabo matano. Likikosekana moja katika hayo mambo matano, hutoka katika utambulisho wa maana ya imani kwa Ahlusunna waljamaa.


Ni ipi dalili ya haya mambo matano?

Amesema mtume Swalla allhu alayhi wasallama (Ya juu yake katika imani ni kusema: (*Laa ilaaha illa allah*) hii ndio dalili ya (Qauli) kusema, (Na ya chini yake ni kuondoa uchafu njiani) hii dalili ya (kutenda kwa viungo) Na (kuwa na haya ni sehemu katika imani.)


Hii ni dalili katika (Amalul-qalbi) matendo ya moyoni. Na kauli yake Allah anasema: (Ni nani miongoni mwenu sura hii imemzidishia imani?) hii aya ni dalili kwamba imani huwa inazidi na ikiwa inazidi basi bila shaka inaweza pia kupungua.

Na yamekuja maelezo yalio wazi kabisa katika hadithi ya mtume rehman na amani zimfikie, akielezea kuhusu kupungua kwa dini (sijapata kuona wapungufu wa akili na dini....) akizungumzia mapungufu ya wanawake.

NGUZO ZA IMANI NI SITA



Nguzo ya kwanza ni kumuamini Allah na inalazimu mambo manne.



NGUZO YA PILI NI KUAMINI MALAIKA

Malaika ni ulimwengu ulio fichika. Na Allah amewaumba kwa nuru. Wanamtii Allah wala hawamuasi, wana roho (Roho takatifu) na wana miili. (Sifa zote njema ni za Allah, muumba mbingu na ardhi, aliyewafanya malaika kuwa wajumbe wenye mbawa mbili mbili, na tatu tatu na nene nne. Huzidisha katika kumba apendavyo) pia wana akili na mioyo. (Hata itapoondolewa khofu kwenye nyoyo zao watasema: mola wetu mlezi kasema nini?) Tuna waamini wao na alichotujulisha Allah kutokana na majina yao. Kama vile: jibril, na Mikail, na Israfil. Pia tunaamini sifa zao (hawamuasi Allah kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrisha) pia tunaamini kazi zao, mfano (wenye kubeba Arshi ya Allah) na tunaamini maelezo ambayo yamekuja kuwaelezea wao kwa ujumla na mmoja mmoja.

NGUZO YA TATU NI KUAMINI VITABU

Inatupasa kuamini kwamba hivyo vitabu ni maneno ya Allah kiuhakika na sio majazi. Na pia yameteremshwa na hayakuumbwa. Na Allah amemteremshia kila mtume kitabu. Na tuna viamini, na vile ambayo ametueleza Allah majina yake na habari zake na hukumu zake, kiu jumla na kimoja kimoja, ambavyo havijafutwa. Na tunaamini kwamba Qur'an imefuta vitabu vyote vilivyo tangulia kabla yake, ambavyo ni Tawrat, Injil, Zabur, Suhufi za Ibrahim na Mussa Rehman na amini ziwafikie.

NGUZO YA NNE NI KUAMINI MITUME

Inatupasa kuamini kwamba wao ni viumbe, hawana sifa za kiuungu kwa chochote. Na wao ni waja wa Allah hawaabudiwa. Allah amewapa utume, na akawapa wahyi, na akawatia nguvu kwa alama mbalimbali, na wao wametekeleza amana waliopewa, wameunasihi umma na wakafikisha ujumbe, na wakapambana kwa ajili ya Allah ukweli wa mapambano. Tunawaamini na wale aliotujulisha Allah majina yao na sifa zao, na habari zao kwa ujumla na mmoja mmoja. Nabii wa kwanza ni Adam amani zimfikie, na mtume wa kwanza ni Nuhu amani zimfikie.

Na nabii na mtume wa mwisho ni Muhammadi rehman na amani zimfikie, na sharia zote zilizotangulia zimefutwa na sharia za Muhammadi rehman na amani zimfikie. Na mitume wenye maazimio na subira ni watano. Wametajwa kwenye sura mbili Shuura na Ahzab (1- Muhammadi rehman na amani zimfikie) (2- Nuhu amani zimfikie) (3- Ibrahim amani zimfikie) (4- Mussa amani zimfikie) (5- Issa amani zimfikie)

NGUZO YA TANO: NI KUAMINI SIKU YA MWISHO

Hii inajumlisha kuamini yote aliyoyaeleza mtume rehma na amani ziwe juu yake. Katika yale yatakayotokea baada ya kifo. Mfano Adhabu za kaburini, kupulizwa baragumu na kusimama kufufuka kutoka katika makaburi yao, na mizani ya kupima matendo ya watu na madaftari ya matendo ya watu, na siratwa na birka ya mtume ambayo waja wema watakunywa, na kuombewa na mtume, na pepo na moto na waumini watamuona mola wao mlezi siku ya kiyama wakiwa peponi, na mengineyo katika mambo ya ghaibu.

NGUZO YA SITA: NI KUAMINI QADARI, KHERI YAKE NA SHARI YAKE

Inapasa ijumuishe nguzo hii kuamini mambo manne.

ELIMU

Kuamini ya kwamba Allah subhaanahu wataala anafahamu kila kitu kwa ujumla na kwa uchambuzi wake.

KUANDIKA.

Kuamini ya kwamba Allah ameandika makadirio ya kila kitu mpaka kitakapo simama kiyama.

MATAKWA.

Kuamini kwamba alichokitaka Allah, basi kimekuwa na kile ambacho hakutaka kiwe hakikuwa na mja ana matakwa lakini matakwa yake yapo chini ya matakwa ya Allah subhanahu wataala.

KUUMBA.

Kuamini kwa mja yeyote ni kiumbe, yeye na matendo yake pia viumbe wote waliobakia. Dalili (Allah ni mwenye kuumba kila kitu). Allah ndiye amewaumba nyie na matendo yenu.

Na hizi daraja nne zilizotajwa hapo juu amezikusanya mtunzi wa kitabu.

- (1) Elimu
- (2) Maandishi ya Mola wetu
- (3) Matakwa yake.
- (4) Na kuumba kwake ambako ni kukipatisha kitu na kukitengeneza.

DARAJA LA TATU NI IHSANI:

Na nguzo yake ni moja tu ambayo ni (Kumuabudu Allah Kama vile unamuona ikiwa humuoni yeye anakuona)

Na ushahidi ni maneno ya Allah mtukufu: (Hakika ya Allah yupamoja na wenye kumcha na watendao mema.) Na kauli yake Allah: (Na mtegemee mtukufu mwenye nguvu mwenye kurehemu. Ambaye amekuona unapo simama. Na mageuko yako kati ya wanao sujudu. Hakika yeye ndio mwenye kusikia, mwenye kujua) Na kauli ya Allah: (Na huwi katika jambo lolote wala husomi sehemu yoyote katika Qur'an wala hamtendi kitendo chochote ila sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo)

DARAJA YA TATU NI IHSANI.

Nayo ni daraja ya juu katika dini, nayo ni nguzo moja na huingia ndani yake daraja mbili.

Ibada ya kuonekana.

Ambayo ni ibada ya kupenda na kutamani na kuwa na shauku na yalio mbele ya Allah. Mfano; Ibada za mitume na manabii amani ziwafikie. Na inawezekana kwa wengine kufikia katika daraja hii.

Ibada ya kumchungu Allah.

Na hii ni ibada ya kumkhofia Allah, na kukimbia maasi kwa ajili ya Allah. Na hatoki nje ya daraja hii muislamu yeyote.

UFAFANUZI: Hii haina maana kwamba mtu mwenye daraja hii ana mapenzi ya Allah tu na hana khofu ya Allah subhaanahu wataala lakini kwenye daraja hii kuna msukumo mkubwa ambao unamsukuma mja katika kufanya ibada. Ambao ni kumpenda Allah subhaanahu wataala Na miongoni mwayo ni kauli ya mtume rehma na amani zimfikie(Kwanini nisiwe mja mwenye kushukuru ?)

DALILI YA HADITHI:

Hadithi ya Jibril iliyo maarufu kutoka kwa Umar radhi za Allah ziwe juu yake amesema:-

Baina za nyakati tulipokuwa mbele ya mtume rehma na amani zimfikie juu yake, siku moja alijitokeza kwetu mtu mmoja mwenye nguo zilizokuwa nyeupe sana, mwenye nywele nyeusi sana, hazionekani kwake athari za kusafiri wala hamtambui yeyote kati yetu mpaka akakaa mbele ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, akayaegemeza magoti kwenye magoti ya mtume rehma na amani ziwe juu yake, na akaweka viganja vyake kwenye mapaja yake na akasema:- Ewe Muhammadi nieleze kuhusu uislamu, akasema mtume rehma na amani ziwe juu yake, (Uislamu ni kushuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na hakika ya Muhammadi ni mtume wa Allah na kusimamisha swala na kutoa zaka na kufunga ramadhani, na kuhiji nyumba ya Allah ukiweza njia ya kuiendea nyumba hiyo).

Akasema (Yule mtu) umesema kweli, Akasema tena;

Nieleze kuhusu Ihsani, Akasema mtume(Ni kumuabudu Allah kana kwamba unamuona ikiwa humuoni yeye anakuona) Akasema (Yule mtu) Nieleze kuhusu kiyama; Akasema (Mtume) Hakuwa mwenye kuulizwa hicho kama anatambua zaidi kuliko muulizwaji. Akasema (Yule mtu) Nieleze alama zake, Akasema (Mtume) Ni mjakazi kumzaa bwana wake, na kuwaona watembea peku, waenda uchi, maskini wachunga mbuzi, wakishindana katika majengo

Akasema Umar, Akaondoka Yule mtu, tukakaa muda mrefu kidogo Akasema (Mtume) (Ewe Umar unamfahamu Yule muulizaji?) Nikasema, Allah na mtume wake ndio wanafaham/wajuzi. Akasema (Mtume) (Yule ni Jibril alikujieni akufundisheni mambo ya dini yenu)

Hadithi hii ni dalili ya nguzo za uislamu na imani na Ihsani kwa kauli ya Mtume rehma na amani zimfikie, (Hakuwa muulizwaji ni mjuzi zaidi kuliko mwenye kuuliza) Maneno hayo ni dalili ya kwamba hafahamu wakati wa kusimama kiyama isipokuwa Allah.

**KAULI YAKE MTUME REHMA
NA AMANI ZIMFIKIE:
(MJAKAZI KUMZAA BWANA
WAKE MAANA YAKE NI:-**

3. Kukithiri kuwaasi wazazi

2. Kukithiri kwa watumwa

1. Kubadilika hali

**Mfalme atamuoa mjakazi
atakuja kumzalia kijana,
atakuwa huyu kijana ni
mfalme baada ya kifo cha
baba yake naatakuja kuwa
bwana wa mama yake**

(Na utawaona watembea peku, waenda uchi, maskini) maana yake ni Mafakiri. (Wachunga mbuzi wanashindana katika majengo) maana yake ni Hali za watu zitabadilika atabadilika huyu fakiri kuwa tajiri mbaya.

**FAIDA ZINAZOPATIKANA KUTOKANA NA HADITHI YA JIBRIL
AMANI ZIWE JUU YAKE.**

1. Mwanafunzi ana haki sita(6) juu yake kuzitekeleza:-

Haki ya nafsi yake, Haki ya walimu wake, Haki za mahala anaposomea, Haki za wenzie, Haki za kitabu chake, Haki ya elimu aliyojifunza.

HAKI YA NAFSI YAKE: Elimu ni ibada (awe na ikhlasi na awe mwenye kufuata) kuwa salafi wa sawa sawa. (salafi ni mfuasi wa wema waliopita) Amukhofie Allah na amchunge, kwa unyenyekevu na kuacha majivuno, kukinai na kuipa nyongo dunia, kujipamba na elimu nzuri kuwa na tabia njema, kudumu katika sifa za uanaume, kuzihama starehe, kupuuza vikao vya upuuzi, kujipamba na upole kuthibiti na kuthibitisha kuwa na hima, kuwa na shauku katika kutafuta, kusafiri, kuifunga elimu, kuhifadhi, uchungaji, kuyapitia aliyoyahifadhi, kujielimisha kwa kuitafuta hukumu kwenye misingi, kujitegemeza kwa Allah, uaminifu wa kielimu. Ukweli.(Kinga au ngao ya mwanafunzi ni kusema sifahamu), kuhifadhi rasilimali(muda), kuipumzisha nafsi, kujielimisha katika elimu mbalimbali, usomaji wa kusahihisha na kudhibiti, kuacha makala zilizo ndefu zaidi, kuuliza vizuri kisha kusikiliza na kufahamu pia kuyafanyia kazi, kufanya majadiliano bila ubishani, kuidurusu elimu, Awe kati ya Qur'an, Sunna na elimu zake, kukamilisha ala za kila fani, matendo, kutokupenda madaraka, na kuacha umaarufu na dunia, kuidhania vibaya nafsi, na uwadhanie vizuri watu, kusafisha elimu (kutetea haki, awe mwenye kuamrisha mema, mwenye kukataza mabaya, mwenye kupima kati ya maslahi na madhara, mwenye kuieneza elimu na kupenda manufaa, kutoa cheo, na kuwaombea mema waislamu katika mambo ya haki na mema) Utukufu, kuhifadhi elimu, kujivutia maslahi sio kudhihaki, kuacha ujuaji na kimbelembele kabla ya kustahiki kwako. Msimamo wako wakutokua na shaka kwa mwenye elimu na kutotofautiana na maulamaa,, hakuna utaifa wala makundi unaoweza kuleta chuki na mapenzi baina ya watu.

- **HAKI YA SHEIKH WAKE:**

Watu kwenye mlango huu wamegawika pande mbili, pia na ya kati na kati. Tutakuja kufahamu kwamba shirki ya kwanza kupatikana katika ardhi ni kwa sababu ya kuchupa mipaka katika haki za watu wema. Hivyo hapana budi tuwe ni wakati na kati katika kuwapenda watu wema si kuchupa mipaka kwao, wala kupoteza haki zao.

- **HAKI YA MAHALA ANAPOSOMEA.**

- **HAKI YA MWENZIE:** Amesema Allah mtukufu (Nyinyi mmekuwa Umma bora uliotolewa kwa watu) Na amesema mtume rehma na amani zimfikie: (Hawi na imani mmoja wenu, mpaka ampendelee ndugu yake inachopenda nafsi yake)

- **HAKI YA KITABU:** Ni kukihifadhi kitabu, kwani Allah subhaanahu wataala ametuneemesha hivi vitabu, hapana budi tuvihifadhi na kuvitunza.

- **HAKI YA ELIMU:** Ni kuithibiti elimu na kuikagua daima, kwa kuirejea mara kwa mara, na kuifanyia kazi, kisha baada ya hapo alinganie kwenye elimu hiyo, kwani hii ni neema na hapana budi kuishukuru hii neema.

2. Miongoni mwa adabu za kuuliza ni kutanguliza swali ambalo hutarajiwa kuwa na manufaa na faida.
3. Ni wajibu kwa mwanafunzi kudumu katika hali nzuri na ya usafi.
4. Baada ya kufa mtume rehma na amani zimfikie, hairuhusiwi kusema (Allah na mtume wake wanajua zaidi) na huruhusiwi kusema (Allah ndie anajua)

Kifungu hiki kimekusanya dondoo kutoka kwa Mtume
Na zikafungamanisha kuanzia jina lake , nasaba yake , umri wake
na chochote alichokifanya katika kazi ya kulingania kwake

Hatuna budi kujua kutoka kwa Mtume mambo muhimu
na miongoni ni :-

UMRI WAKE.

Anao umri wa miaka sitini
na mitatu (63) miongoni
mwa hiyo miaka arobaini
(40) kabla ya kpewa utume ,
na miaka ishirini na mitatu
baada ya kupewa utume

JINA LAKE NA NASABA YAKE.

Yeye ni Muhammad mtoto
wa Abdallah , na Abdallah
ni mtoto wa Abdil-
mutwalib, na Abdil-
mutwalib ni mtoto wa
Hashim , na Hashim
katokana na kabila la
makuraishi lililotokana na
waarabu katika kiazazi cha
Ismail mtoto wa Ibrahimu
kipenzi cha Allah (amani
ziwe juu yake)

MSINGI WA TATU :

KUMJUA MTUME WENU MUHAMMAD.

Yeye ni Muhammad mtoto wa
Abdallah , na Abdallah ni mtoto wa
Abdil-mutwalib, na Abdil-mutwalib ni
mtoto wa Hashim , na Hashim
katokana kabila la makuraishi
lililotokana na waarabu katika
kiazazi cha Ismail mtoto wa Ibrahimu
kipenzi cha Allah (amani ziwe juu
yake)

Anao umri wa miaka sitini na mitatu
(63) miongoni mwa hiyo miaka
arobaini (40) kabla ya kupewa utume
, na miaka ishirini na mitatu baada ya
kupewa utume.

Alipewaunabii kwa kuteremshiwa
suratul (ALAQ)

Na alipewa utume kwa kutershiwa
suratul (MUDDATHIR)

Umegawanyika muda wa utume wake

katika sehemu :-

MUDA ALIOISHI MAKKA

Alidumu kwa muda wa miaka mitatu

MUDA ALIOISHI MADINA

Alidumu kwa muda wa miaka kumi

Je yeye ni Nabii au Mtume?

Yeye ni Nabii na Mtume Alipewe unabii kwa tamko la (SOMA) na kupewa utume kwa tamko (Ewe mweye kujigubika)

DONDOO ZINAZOHUSU MWENENDO WA MTUME

Allah alimtuma Mtume kuwaonya watu na shirki , na kulingania katika Tauhid

dalili ni kauli ya Allah mtukufu : ((Ewe uliejigubika) (simama na uonye) . (na mola wako mlezi mtukuze) . (na nguo zako zisafishe) (na yaliyo machafu yahame) (wala usitoe kwa kutarajia kuzidishiwa .

maana ya (simama uonye) uonye kutokana shirki na ulinganie kwenye Tauhid.

(na mola wako umtukuze) mtukuze kwa Tauhid (kumpwekesha) .

(na nguo zako zisafishe) safisha matendo yako kutokana ushirikina .

(na yaliyo machafu yahame) masanamu .

Na kahama kwake ni kuyaacha na kujiweka mbali nayo na watu wake .

Ilichukuwa kazi hii ya kulingania kwa mtume miaka kumi , na baada ya miaka hiyo kumi alipandishwa mbinguni , na akafaradhiwa swala tano , na aliswali akiwa Makka muda wa miaka mitatu , na baada yake aliamrisha kuhama kwenda madina .

Ulikua ulinganizi katika muda aliokuwa Makka umejikita katika Tauhid , na ulingazi ulikuwa ni kuupuuza ushirikina na kujitakasa na na ibada kwa ajili ya Allah peke yake , na uliendelea ulinganizi huu kwa muda wa miaka mitatu .kisha akapewa amri bwana mtume kuhama kwenda MADINA , vile vile aliendelea na kazi ya da'awa hali ya kusimamisha Tauhid kwa kuongeza kile kilicho teremshwa katika sheria zilizobaki katika dini miongoni mwa Ibada mbali mbali na matendeano pamoja na mambo ya kimaisha .

Ispokuwa Hakika mwenye kuona katika mwenendo wake Mtume katika kulingania hakika ulinganizi wa Tauhid unabaki kuwa ni wenye kulazimiana nae mpaka pale Allah alipomfisha , na jambo hili ni majibu ya wazi katika kuwarudi kwa kila mwenye kuwapa nyongo watu katika kujifundisha tawheed na kudai ya kuwa tawheed haihitajii mtu kujifundisha ispokuwa kwa dakika zenye kuhesabika .

Kauli yake رَحْمَةُ اللَّهِ (alipandishwa mbinguni) tunapata faida ya :-

- 1- Hakika alichokisema Mtume miongoni mwa mambo yasiyoonekana , sisi tunasema : tunaamini , tunasadikisha na tumejisalimisha .
- 2- Umihimu wa swala tano zilizo faradhiwa ,kwa nanmna ya kuwa Allah mtukufu alizifaradhiwa mbinguni.

Hijra: Ni kuhama kutoka mji wa shirki kwenda mji wa uislamu. Na hijra imekuwa ni faradhi juu ya huu umma. Kutoka mji wa shirki kwenda mji wa kiislamu kuhamia huku kutabakia hadi kitakapo simama kiamama. Amesema Allah subhanahu wataala “Hakika malaika atawaambia wale ambao wamewafisha nao wamejidhulumu nafsi zao: Mlikua vipi? Watasema: Tulikuwa tunaonewa. Watawaambia: Kwani ardhi ya Allah haikuwa na wasaa wa kuhamia humo? Basi hao makazi yao ni jahanam, nao ni marejeo mabaya kabisa, isipokuwa wale waliokuwa wanyonge miongoni mwa wanaume na wanawakena watoto wasio na uwezo wala hila na kuongoza njia ya kuhama.

Basi hao Allah akawasamehe na Allah ni mwingi wa kusamehe na mwinyi wa maghfira. Na kauli yake Allah mtukufu “Enyi waja wangu mlio amini hakika ardhi yangu ina wasaa basi mniabudu mimi peke yangu” amesema Imaam Al-Bagh’awi Allah amreham: “Sababu ya kuteremka ayah ii ni kwa waislam wa Makkah ambao hawakuhamia. Allah aliwaita kwa jina la (Iman)

Na dalili ya hijra kutoka katika sunnah ni kauli ya mtume swalalahu walayhi wasalam “Hakutakoma kuhama vingineyo mpaka iishe toba na haitaikoma toba mpaka lichomoze jua upande wa magharibi”

Kauli ya Mtume swalalahu walayhi wasalam (Hakuna kuhama baada ya ufunguzi wa mji wa Makka (Yaani kutoka Makka kwenda Madina na katika hili kunaisha kutoka kwa mtume swalla llahu alayhi wasallama Hakika mji wa Makka haiwezekani tena ukawa mji wa kikafiri.

KUNAGAWANYIKA KUHAMIA KATIKA SEHEMU KUU TATU.

Kuhama kwenda kuliendea lile ambalo ameliwajibisha Mwenyezi Mungu.

Miongoni ni kufanya Amal, na muda wa kufanya a’mal na sehemu ya kufanya a’mal

Kuhama kutoka Makka kwenda Madina kuhama huku hakupo kumekoma baada ya ufunguzi wa mji wa Makka

Kuhama kutoka katika mji wa kikafiri kwenda mji wa kiislamu hukumu yake ni wajib

Neno a’mal

Kila jambo aliloliharamisha Allah subhanahu wataala na jambo kubwa aliloliharamisha ni shirki.

A’amil: Ni makafiri na wanafiki na wengineo.

Zamaan: Ni kuhama kwa muda ambao wanakusanyika makafiri.

Makaan: Sehemu: Ni kuhama sehemu ambayo wanakusanyika sehemu hiyo makafiri.

Inakoma tawbah kwa moja ya mambo mawili.

1. Ni kuchomoza jua kutoka magharibi

2. Kufikwa na umauti. Amesema Allah subhanahu wataala

“ Wala hawana toba wale wafanyao maovu mpaka yatakapomfikia mmoja wao umauti, kisha hapo akasema. Hakika mimi sasa nimetubia, wala wale wanaokufa na hali yao ni makafiri hao tumewaandikia adhabu chungu”

Kauli ya mtume (*swalla llahu alayhi wasallam*) “ Hamna Hijra baada kuukomboa mji Makka” yaani kutoka Makka kuhamia Madina , ni ishara kwamba mji wa Makka haiwezekani tena kurudi kwa mji wa kikafiri .

Baada ya kuweka makazi mji wa madina akapewa sheria zilizobakia katika uislamu mfano : Zaka, Swaum, na Hija, Jihadi na Adhana , kuamrisha mema na kukataza maovu na mengineyo miongoni mwa sheria za kiislamu .

Kazi hii aliifanya kwa muda wa miaka kumi na baada ya miaka hiyo alifishwa (Rehma na amani ziwe juu yake)

Na hii dini yake ipo , na katika dini hii , hakuna kheri yoyote ila ameifundisha na wala shari yeyote ila ameitahadharisha.

Na kheri ambayo ameifundisha kuitekeleza ni Tawheed na mambo yote anayoyapenda Allah na kuridhia .

Ama shari aliyoitahadharisha ni Shirki na mambo yote anyoyachukia Allah na kuyakataa.

1- Anasema shikh **IBN- UTHAIMIN** Rehma za Allah ziwe juu yake:-

Zaka ilifaradhishwa mwanzo katika mji wa Makka lakini hikupangiwa viwango vyake wala kukdriwa uwajibu wake .

Na katika mji wa madina ndiko kulipangwa viwango vyake na kukadirwa uwajibu wake .

2- Alifishwa Mtume (Rehma za Allah ziwe juu yake) katika mwaka wa kumi baada ya kuhama , na alizikwa katika chumba cha mkewe bibi Aisha (radhi za Allah ziwe juu yake)

3- Hakuna kheri yoyote ila ameifundisha katika umma na wala shari yeyote ila ameitahadharisha.

Hatuna budi kuthibitisha kuwa hakika ametekeleza amana , amefikisha utume , amenasihi umma , amepigania jihadi dini ya Alla ukweli wa kupigania, na akatuacha katika mwanga usiku wake kama mchana wake hakuna atakaepotea ila atakuwa mwenye kuangamia.

MAMBO YALIYO HARAMISHWA

Shirki kubwa

hii inamtoa mja katika mila ya uislamu

Shirki ndogo

hii haimtoi mja katika mila ya uislamu

Dhambi kubwa

ni kila aina ya dhambi iliyo andikiwa adhabu maalum

Dhambi ndogo

ni kila jambo lililoharamishwa na halijaandikiwa adhabu maalum

Allah alimtuma mtume wake kwa watu wote na akalazimisha twaa yake kwa viumbe wa aina mbili nao ni majini na watu. Nadalili ni kauli yake Allah mtukufu (Sema waambie watu hakika mimi ni mtume wa Allah kwenu nyinyi wote) 1.

Na Allah akaikamilisha yake kupitia Mtumewake Na dalili ni kauli yake Allah mtukufu: (Leo nimewakamilishia dini yenu na nimezitimiza neema zangu juu yenu na nimeridhia kwenu ya kwamba uislamu ndio dini)

Na dalili inayoelezea juu ya kufa kwake mtume ni kauli ya Allah mtukufu:

(Hakika wewe utakufa na wao watakufa kisha bila shaka siku ya qiyama mtalumbana mbele ya mola wenu)

Alitumwa mtume Muhammad swalalahu walaihi wasalam kwa watu wote na zikafutwa sheria zote zilizo kuwepo kabla yake .

basi mayahudi na manasara (makafiri) kuanzia zama za mtume swalalahu walaihi wasalam na katika zama zetu hizi leo pindi itakapowafikia da'awa na wasiingie katika dini basi hao watakua ni makafiri hata kama wakiwa na sifa kama za wale aliekua nao nabii Mussa na nabii Issa amani za Allah ziwe juu yao.

Na miongoni mwadalili ya hayo ni

1. kauli ya Allah alie tukuka (Sema: enyi watu wa kitabu! Njooni kwenye neno lililo sawa baina yetu na nyinyi: ya kwamba tusimuabudu yeyote isipokuwa Allah na wala tusimshirikishe na chochote ,

2. kauli ya Allah mtukufu (piganeni na wale wasio muabudu Allah na siku ya mwisho wala hawaharamishi aliyo haramisha Allah na mtume wake , wala hawashiki dini ya haki miongoni mwa waliopewa kitabu.

3. kauli yake mtume swalalahu walaihi wasalam (Naapa kwa Yule nafsi yangu ipo mikononi kwake hato sikia kutoka kwangu myahudi yeyote wala mnasara yeyote (mkristo) kisha asiniamni isipokua atakua mtu huyo ni miongoni ya watu wa motoni).

- 1- Watu wote wataonja mauti bila shaka na ni wenye kufufuliwa siku nzito hiyo nayo ni siku ya qiyama na ni wenye kuhesabiwa na kulipwa kulingana na amali yake mja.
- 2- mwenye kupinga kufufuliwa na kuhesabiwa ni kafiri kwa sababu mtu huyo amepiga nguzo miongoni mwa nguzo za imani.
- 3- Nuhu amani za Allah ziwe juu yake ni mtume wa kwanza na dalili ni kauli yake Allah mtukufu(Hakika sisis tumekuletea wahy kama tulivyo mpelekea Nuhu na manabii waliokuja baada yake).

Ama nabii wa kwanza ni nabii Adam na dalili nikauli yake Allah mtukufu(Hakika mtume swalalahu walaihi wasalam aliulizwa kutokana na Adam je yeye ni nabii?akasema:ni nabii mwenye kusemeshwa na Allah).

Na mwisho wa manabii ni nabii Muhammad swalalahu walayhi wasalam na dalili ni kauli yak e Allah mtukufu (Muhammad si baba wa yeyote katika waume zenu bali ni mtume wa Allah na wa mwisho katika manabii)

Basi kila mwenye kudai unabii au utume baada ya mtume Muhammad swalalahu walayhi wasalam basi mtu huyo atakua ni muongo na ni kafiri ,na kila mwenye kumsadikisha mtu huyo mwenye kudai unabii basi na yeye atakua ni kafiri mfano wake.

Na watu pindi watakapo kufa watafufuluwa na dalili ni kauli yake mtukufu(Kutokana na ardhi tumekuumbeni na humohumo tutakurudisheni,nakutokea humo tutakutoeni mara nyingine)

Na kauli yake Allah mtukufu(Na Allah ame kuotesheni katika ardhi kama mmea.kisha atakurudisheni humo na atakutueni tena)

Baada ya kufufuka mtahesabiwa na mtalipwa kwa matendo yenu .

Na dalil ni kauli yake Allah mtukufu(Ni vya Allah vyote vya mbinguni na aridhini ili awalipe walio tenda ubaya kwa walio yatenda,na walio tenda mema awalipe mema)

Na mwenye kupinga kufufuka ni kafiri dalili ni kauli yake Allah mtukufu(waliokufuru wanadai kwamba hawato fufuliwa,sema :kwani?naapa kwa mola wangu mlezi!hapana shaka mtafufuliwa kasha hapana shaka mtaambiwa mliyotenda.na hayo ni mepesi kwa Allah)

Na aliwatuma Allah mitume wake wote kutoa bishara njema kwa watu wao na kuwahofisha na moto,na dalili nii kauli yake Allah mtukufu(mitume hao ni wabashiri na waonyaji)

Mtume wa kwanza kwa hao mitume ni Nuhu amani za Allah ziwe juu yake na wa mwisho ni mtume Muhammad swalalahu walaihi wasalam na ni wa mwisho kwa manabii.

Na dalili inayo onyesha kwamba mtume wakwanza ni Nuhuamani ziwe juu yake ,kauli ya Allah mtukufu(Hakika sisi tumekuletea wahy wewe kama tulivo wapelekea wahy Nuhu na manabii wengine waliokua baada yake)

Allah amewaamrisha waja wake wote kumpinga shetani na kumuamini Allah,amesema mwanachuoni IBNUL-QAYYIMU Allah amrehemu;(ushetani :ni kitendo cha mja kuvuka mipaka katika kuabudu au kufata au kutiiwa)

Na katika kila umma Allah amepeleka mtume kuanzia mtume Nuhu subhanahu wataalampaka mtume Muhammad swalalahu walaihi wasalam na kazi yao ilikua ni kuamrisha waja kumuabudu Allah pekee na kuwakataza juu ya kumuabudu shetani.Na dalili ni kauli yake Allah mtukufu (Hakika tumempeleka mitume katika umma zote kwamba wamuabudu Allah na wajiepushe na shetani)

Na mashetani ni wengi sana na viongozi wao ni watano(5):Ibilisi alie laaniwa na Allah,(2)ni yule anae abudiwa na waja hali ya kuwa yupo radhi(3)na Yule mwekuwaita watu katika ibada yake binafsi(4)na Yule mwenye kudai kujua elimu ya ghaibu(mambo yasio onekana) (5) na Yule anae hukumu tofauti na alivyo teremsha Allah mtukufu.Na dalili ni kauli yake Allah (Hakuna kulazimishana katika dini kwani uongofu umesha pambanuka na upotofu.basi anaemkataa shetani na kumumini Allah bila shaka amekamata kishiko kisicho vunjika)

Na hii maana ya kwamba Hakuna apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah.

katika hadithi(Msingi mkubwa katika uislamu na nguzo zake ni swala na kilele cha juu ni jihadi katika njia ya Allah

Allah alituma mitume na manabii kuwabashiria watu pepo na kuwahofisha na moto na wote hao kazi yao ilikua juu ya kumpwekesha Allah subhanahu wataala na kupambana na shetani na ushirikina kwa namna zote na dalili ni kauli yake Allah mtukufu (Na kwa hakika kwa kila umma tumewatumia mtume kwamba muabuduni Allah na muogopeni shetani).Na kwa hakika kila umma tuliutumia mtume wake:maana yake kila watu (wamuabudu Allah) na (wampwekeshe) na (wajiepushe na shetani)—maana yake mfanyeni shetani katika upande na nyinyi muwe katika upande mwengine.Na hii itakua ni njia ya juu katika kumkemea shetani na kumuweka mbali na wao nahilo jambo ni lakujihakikishia usafi kutokana na shiriki na watu wake ,na ameamrisha Allah kwa waja wake wote kumpinga shetani na kumuamini Allah na hapana shaka ndani yake ,Allah anasema(Atakae mpinga shetani na kumuamini Allah).

Na ushetani:ni mja kuvuka mipaka katika kuabudu(kama kuabudu mawe na miti) au kufuata (kama kuwafata wanachuoni waovu) au kuwatii (kama viongozi walio nje nay a twaa ya Allah.

Na mashetani ni wengi sana na viongozi wao ni watano(5) na kiongozi wa juu kabisa ni Iblisi Allah amemlaani na miongoni mwa mlango wa kutolea habari na atakae abudiwa na akiwa radhi na yeyote Yule atakae lingania watu katika ibada yake binafsi na Yule mwenye kudai kujua elimu ya ghaibu(mambo ya sio onekana) na atakae hukumu kinyume na alivyo teremsha Allah.

KUKUFURU KWA KUFANYA JAMBO ASILOTEREMSHA ALLAH

KUFURU KUBWA

Mwenye kuitakidi ya kwamba hukumu ya mtu ni sawa na hukumu ya Allah au au zaidi yake .

KUFURU NDOGO

Mwenye kuitakidi ya kwamba hukumu bila kufuata aliyoteremsha Allah ni batili , lakini anahukumu kwa matamania au kuapenda uongozi au au kwa sababu nyingine yeyote .

IMAMU IBNUL- QAYYIM AMEIGAWA JIHADI KATIKA SEHEMU

JIHADI YA NAFSI.

Inakuwa kwa kutafuta elimu ,kuifanyia kazi katika njia sahihi katika njia ya Allah .na kusubiri

JIHADI YA SHETANI.

Inakuwa kwa kuacha yenye kutatiza (shirki na uzushi)

Na katika yenye kutatiza kuna makubwa na madogo

JIHADI YA MAKAFIRI NA WANAFIKI

Inakuwa kwa kuudhibiti moyo , ulimi , mali na nafsi .

JIHADI YA VIONGOZI WA DHULMA , WAZUSHI NA WAPINGAJI

Inakuwa kwa kutumia mkono , ulimi na moyo .

MWISHO

Ni wajibu kwa kila mwenye akili kuzingatia huu msingi ,na kuuchunga kwa uangalifu maalum sana , kwa kuwa imekusanya misingi mikuu anayohitaji kila mwanadamu kaburini kwake

Kwa haya yote ALLAH ni mjuzi zaidi , rehema na amani zimuendee mtume Muhammad

MISINGI MITATU (NAYO KWA MUKHTASARI MASWALI YA KABURINI) , DALILI ZAKE , KWA NINI TUNASOMA TAWHEED ? KWA NINI TUNASOMA MISINGI MITATU ?

MAS'ALA MANNE NA DALILI ZAKE(SURATUL-ASR)

ELIMU

Kumjua Allah , na kumjua mtume wake na kuijua dini ya kiislamu kwa dalili .

(kwa maana ya : **MISINGI MITATU**)

KUIFANYIA KAZI ELIMU

“ Inaita elimu kwa kuifanyia kazi , basi ikiwa mtu ataitikia itakuwa kheri kweke na kama si hivyo inaondoka.”

“ Namweye elimu kwa elimu yake aspoifanyia kazi Atakuwa ni mweye kuadhibiwa kabla ya wenye kuabudu masanamu

KULINGANIA WATU KWA HIYO ELIMU

MASHARTI YA KULINGANIA: Utakaso . Elimu ya kisheria . Kujua hali ya mwenye kulinganiwa , Hekima . Subra

Jambo la kwanza kulinganiwa ni Tauhid , na hii ndio kazi waliofanya Manabii na Mitume .
Na nafasi iliyokuwa ya juu kabisa katika kulingania ni Tauhid na kupinga shirki

KUWA NA SUBIRA JUU YA MAUDHI NDANI YAKE.

Kusubiri katika kumtii Allah kama (kuswali) na kujizuia kutokana maasi kama (riba)
Na juu ya yote aliyoyakadiria Allah yenye kuumiza kama (ufakiri)

Maana yake : kusubiri katika kutafuta elimu kasha katika kuifanyia kazi na kasha kuilingania .

MAS'ALA MATATU

Tauhid ya malezi (kumpwekesha Allah katika malezi hapana budi kupwekesha vilevile katika uungu wake)

Na kumpwekesha katika majina na sifa zake

Kusubiri katika kumtii Allah kama (kuswali) na kujizuia kutokana maasi kama (riba)
Na juu ya yote aliyoyakadiria Allah yenye kuumiza kama(ufakiri)

Tauhid ya uungu (utakaso) , na hakika Alla haridhii kushirikishwa pamoja nae yeyote katika ibada yake , si Malaika alie karibu wala Nabii mwenye kutumwa .

Kujisafisha na kujiweka mbali na shirki na watu wake : kwa moyo (kuchukia) na ulimi

“ HAKIKA MIMI NIKO MBALI NA VILE MNAVYOVIBUDU”

MISNGI MITATU (NAYO KWA MUKHTASARI MASWALI YA KABURINI) , DALILI ZAKE , KWA NINI TUNASOMA KWA NINI TUNASOMA MISINGI MITATU ?	SABAU ZA KUSOMA TAUHID	AI-HANAFIYA -Ni mila iliyo kuwa mbali na shirki iliyo jengwa katika misingi ya Tauhid iliyotakasika.
		MAANA YA TAUHID KILUGHA: Neno hili limetokana na kitendo ;alipwekesha,anapwekesha,kupwekesha,kupwekesha kitu ni kufanya kitu kuwa ni kimoja .
		MAANA YA TAUHID KILUGHA: Ni kumfanya Allah kuwa ni mmoja katika
		AINA ZA TAUHID. 1-Tawheed ya malezi;Ni kumpwekesha Allah kwa vitendo vyake ,kuumba,ufalme na uendeshaji.2- Tauhid ya uungu;Ni kumpwekesha Allah katika ibada na katika vitendo vya waja.Tawheed ya sifa ;Ni kumpwekesha Allah kwa majina aliojiita yeye mwenyewe katika kitabu chake au kwa maneno ya mtume wake swalalahu walayhi wasalam na hayo kwa kuthibiti yale alioyathibitisha na kuyakanusha aliye ya kanusha bila kuzidisha au kupunguza na bila ya kufananisha.
		Maana ya shirki ; Ni kulingania kwa asiyekua Allah alietukuka,nah ii ni dhambi kubwa aridhini
	MISINGI MATATU	KUMJUA ALIYE TUKUKA ; Mola mlezi ni Yule mwenye kuabudiwa,Aina za ibada,Hukumu kwa mwenye kufanya chochote katika aina za ibada kwa asiye kuwa Allah pamoja na dalili zake
		KUJUA DINI YA KIISLAM KWA DALILI; Kujua uislam,misingi ya dini ,nguzo za uislam,kujua shahada ,nguzo za imani ,sehemu ya imani,dalili za misingi ya imani dalili za kiama.
		KUMJUA MTUME WAKE; Kuzaliwa kwake umri wake ,unabii wake ,utume wake,mji wake hekma ya kupewa kwake utume,muda aliolingania tawheed,safari ya ISRAA,na MIRAJI,wap na lini ilifundishwa swal,kuhama na lini na ipi hikma yake ,wakati gani sheria zilizo bakia zilianza kufanya kazi,muda wa kulingania ,na kufariki kwake,mambo alio kuja nayo katika dini kuenea kwa utume wake kwa viumbe wa aina mbili kukamilika kwa dini na kwa kutumia neema.

MISINGI MITATU (NAYO KWA MUKHTASARI MASWALI YA KABURINI) , DALILI ZAKE , KWA NINI TUNASOMA TAUHID? KWA NINI TUNASOMA MISINGI MITATU ?	MWISHO		Kufufuka baada ya kufa na kuhesabiwa kwa matendo, ukafiri kwa mwenye kupinga kufufuka , wadhifu wa mitume na kulingana kwao, wa kwanza kwa mitume na wa mwisho wao, nguzo za Tauhid; ukafiri wa shetani na kumuamini Allah, kumjua shetani, viongozi wa mashetani, sifa ya ukafiri wa shetani maana ya neno (Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah uislamu ndio iniini wa dini. msingi wa	
	AINA ZA JIHADI	JIHADI YA NAFSI	Hii jihadi inakua kama ilivyo elezwa katika suratul-Asri (Ni elimu, kuifanyia kazi hiyo elimu, na kulingania elimu, pia na kuwa na subira)	
		JIHADI YA SHETANI	MATAMANIO YA NAF SI	Madhambi makubwa (Ni kila dhambi ilivopangiwa adhabu vake maalum)
			MAMBO YENYE KUTAMANISHA	Madhambi madogo (Ni kila lililo haramishwa likawa halikupangiwa adhab maalum adhabu vake maalum)
				Shiriki kubwa (Ni ile yenye kumtoa mtu katika mila ya uislamu. Shiriki ndogo)
				Uzushi
		JIHADI YA MAKAFIRI NA WANAFIKI	Jihadi hii inakuwa kwa moyo, kwa ulimi, kwa viungo na kwa mali	
		JIHADI YA VIONGOZI WA DHULMA , WAZUSHI NA WAPINGAJ	Jihadi hii inakuwa kwa moyo, kwa ulimi na kwa viungo .	

TWAGHUTI

Ni kuvuka mipaka yake mja katika kuabudu kama vile (kuabudu mawe na miti) au mwenye kufuatwa (kama vile kuwafuata wanachuoni waovu) au mwenye kutiiwa (kama vile kuwatii viongozi walio nje na twaa ya Allah.

Mashetani niwengi ,na viongozi wao wapo aina tano 1. Iblisi alie laaniwa na Allah.(na shekh hapa tambua hakika si vinginevyo amemlaani kwa kumwambia)

2.Mwenye kuabudiwa na akawa radhi 3. mwenye kudai kujua mambo ya sio onekana.4.mwenye kulingania watu katika ibada yake ,5mwenye kuhukumu kinyume na alivyo teremsha Allah .

ALLAH NI MJUZI ZAIDI

Rehma na amani ziwe juu yake mtume Muhammad syeye na ahli zake na Maswahaba wake.

MTIHANI WA MISINGI MITATU NA DALLI ZAKE.

***CHAGUA JIBU KUTOKA NDANI YA YALE YAMO KWENYE MABANO**

1. misingi mitatu ni kwa muhtasari maswali ya kaburi(ndiyo-hapana)

2.mtunzi wa hiki kitabu MISINGI MITATU amemlinga n mwenye kukisoma hiki kitabu katika (sehemu mbili –sehem tatu)

3-vimesifika vitabu vya mtunzi kitabu hiki kwa(sentensi nyepesi-kwa ujumla na ufafanuzi-kwa dalili kutoka katika Qur-an na sunna)

- kumuombea mwanafunzi- kujibu shubha za kisasa h – uwingi wa sherhe katika vitabu hivyo - kuleta maswali muhimu na majibu yake - Allah kuvijaalia vitabu kuwa ni vyenye kukubalika – yote yaliyotangulia .

4-inawezekana kugawa mpangilio wa asili ya kitabu hiki cha misingi mitatu katika vipengele (5, 6)

5-Kusoma Tawheed (ni faradhi itoshelezayo-faradhi ya lazima)

Dalili ya misingi mine(suratil-asr(surai-iklas)

6-Mwenye kujifunza kasha asiyafanyie kazi aliyojifunza mfano wa (manasara- mayahudi-wote wliotangulia)

7-Subra(inatosha kusimisha hoja-inatosheleza sura zilizobakia)

8-Maana ya kauli ya imam Shafi katika suratul asri ya kwamba hiyo sura(inatosha kusimamiaha hoja inatoshelezasura zilizobakia)

9-Mwenye kuamini aina moja ya tawheed bila ya kuamini aina zilizo bakia hawezi kuwa na imani ya Tawheed(sahihi-kosa)

10-mwenye kujitakasa na shirki na jamii yake kunakuwa kujitakasa huko ni kwa (moyo,ulimi na viungo-kujitakasa na matendo na mwenye kutenda-vyote)

11-Maana ya neno (misikiti)katika jina lake Allah (Na hakika misikiti ni ya Allah) maana yake(misikiti iliyojengwa –viungo vya kusujudia-Ardhi ammbayo husujudiwa juu yake – majibu yote sawa)

12-Mwenendo wa wema waliotangulia ni (dalili kasha ndio itikadi-ni itikadi kasha ndo dalili)

13-Mwenye kupotea miongoni mwa wanachuoni wetu basi huko ni kufanana(mayahudi-manasara)

14-Mwenye kupotea miongoni mwa waaumini wetu basi huko ni kufanana na (mayahudi-manasara)

15-mambo matatu ndio misingi ya misingi Mitatu(sahihi-kosa)

16-Inagawanyika dua kwenye (dua ya ibada,na dua ya maombi na uhalisia wa mtu,na dua ya hali ya kusoma)

17inagawanyika dua ya mambo kwenye(sehem-sehem nne)

18- Wamegawanyika watu katika kuitikadi sababukwenye(vigawanyo viwili na katika – shirki kubwa na ndogo na inavyofaa)

19-kuna sahihi kujiokoa kwa kutumia viumbe(bila sharti kwa kile anocho kiweza kwa masharti manne)

20-Maana ya neno (Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokua Allah ni(Muweza juu ya kumba –Hakuna wa kuabudiwa isipokua Allah –yote yalio tangulia ni majibu)

21-kujikurubisha na dini nyingine (inajuzu-kukubwa-ukafiri)

22-Dalili zenye kuonesha uwepo Allah kwa ujumla dalili hizo ni (Nyingi-Nne)

23-Je malaika wana mioyo(ndio-hapana)

24-Uhusiano wa Tauhid na imani ni kwamba imani ni jambolililo kusanya vitu vyote,na Tauhid ni sehem katik iman(sahihi-kosa)

25-Nguzo za imani (5,6,8)

26-Washirikina wanasehemu katika kumuabudu Allah(sahihi-kosa)

27-Maana ya neno (misikiti)katika jina lake Allah (Na hakika misikiti ni ya Allah) maana yake(misikiti iliyojengwa –viungo vya kusujudia-Ardhi ammbayo husujudiwa juu yake – majibu yote sawa)

14-Mwenendo wa wema waliotangulia ni (dalili kasha ndio itikadi-ni itikadi kasha ndo dalili)

15-Mwenye kupotea miongoni mwa wanachuoni wetu basi huko ni kufanana(mayahudi-manasara)

16-Mwenye kupotea miongoni mwa waaumini wetu basi huko ni kufanana na (mayahudi-manasara)

17-mambo matatu ndio misingi ya misingi Mitatu(sahihi-kosa)

18-Inagawanyika dua kwenye (dua ya ibada,na dua ya maombi na uhalisia wa mtu,na dua ya hali ya kusoma)

1-inagawanyika dua ya mambo kwenye(sehem-sehemne)

2-Wamegawanyika watu katika kuitikadi sababukwenye(vigawanyo viwili na katika – shirki kubwa na ndogo na inavyofaa)

21-kuna sahihi kujiokoa kwa kutumia viumbe(bila sharti kwa kile anocho kiweza kwa masharti manne)

22-Maana ya neno (Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokua Allah ni(Muweza juu ya kumba –Hakuna wa kuabudiwa isipokua Allah –yote yalio tangulia ni majibu)

23-kujikurubisha na dini nyingine (inajuzu-kukubwa-ukafiri)

24-Dalili zenye kuonesha uwepo Allah kwa ujumla dalili hizo ni (Nyingi-Nne)

25-Je malaika wana mioyo(ndio-hapana)

26-Uhusiano wa Tauhid na imani ni kwamba imani ni jambolililo kusanya vitu vyote,na Tauhid ni sehem katik iman(sahihi-kosa)

27-Nguzo za imani (5,6,8)

28-Washirikina wanasehemu katika kumuabudu Allah(sahihi-kosa)

- 29-Mwenye kuabudiwa kinyume na anavyo abudiwa Allah na akaridhia huyo (ni shetani – siyo shetani)
- 30- Mwenye kumpwekesha Allah kwa kuuendesha ulimwengu huuna kuteremsha mvua hiyo tawheed (uungu-mlezi na majina masfi)
- 31-Miongoni mwa yanayo pingwa na misingi ya Tawheed ni(shirki –ndogo-na uzushi)
- 32-Miongoni mwa yalio wajibishwa ni pamoja na kuwatendea wema wazazi wawili(sahih-kosa)
- 34-Miiraji ni safari ya mtume kutokea makkah kwenda nyumba takatifu pale palestina(sahihi-kosa)
- 35-Alitumwa mtume Muhammad swalalahu walayhi wasalam kwa (watu wake maalumu-viumbe wa aina mbalimbali)
- 36-Nabii Muhammad swalalahu walayhi wasalam alikufa (manabii hawafi)
- 37-Mwenye kupinga kufufuliwa amekufuru kwa ukafiri(mkubwa-mdogo)
- 38-Dini ya manabii ni moja (kila nabii alikua na dini yake)
- 39-kuha (kulikoma baada ya ufunguzi wa mji wa makkah-bado kuendelea mpaka siku ya qiama)
- 40-hijra(kuhama kutoka mji kutoka mji wa ukafiri kwenda mji wa kiislam –kuachana nay ale aliyo ya haramisha Allah
- 41-Dini ya kiislamu imekamilika isipokua yale yaliopo ni miongoni mwa ndoto za waja wema(sahihi-kosa)
- 42-Kfanya ibada isiyo ya Allah ni shirki (kubwa-ndogo)
- 43-Hapana budi katika kutofautisha baina ya hukumu ya kitendo na hukumu ya mtendaji(sahihi-kosa)
- 44-Nabii wa kwanza ni(Nuhu(s.a)-Adam(s.a))
- 45-Nabii wetu swalalahu walayhi wasalam ni(nabii-mtume)

CHAGUA KUTOKA ORODHA YA MANENO YALIYO SAHIHI NA ORODHA YA PILI

ORODHA YA KWANZA	NAMBA	NAMBA	ORODHA SEHEMU YA PILI
Tawheed kilugha		1	Kauli ya Ah-mad:(utakapo muona kafiri amefumba macho kwa kuogopa kumuona adui wa Allah.
Tawheed kisheria		2	Inafungamana imani hii kwa kile linalo kuwa baada ya mauti.
Tawheed ya uungu		3	Ni kutamka kwa ulimi na kuamini kwa moyona kuto leglega kwa vitendo na nguzo(imani)inayo ongezekwa kwa twaa na ina pungua kwa maasi. Ni uislamu na imani na ihsani.
Tawheed ya malezi		4	
Tawheed ya majina na sifa		5	Kwa ajili ya Allah na asiye kuwa Allah.
Hanifinya mlingano na kwanza na ni amri katika qur an		6	Wajibu na inajuzi na haramu.
		7	Ni kisheria na kihisio.
Shirki		8	Maswali ya kaburini.
Kutegemea		9	Ni elimu na amali na ulinganizi na subra.
Sharti za kukubaliwa ibada		10	Ni kujitakasa na kufata.
Masaail manne kwa muhtasari		11	Ni uaminifu wa kuegemea kwa Allah pamoja na ujasiri wake na kuchukua sababu.
		12	Ni khofu iliyojengwa juu ya elimu na kwa ukubwa wa Yule anaemugopa na ukamilifu wa mamlaka yake.
Masaail matatu kwa muhtasari		13	Ni mfano na uasawa.
Misingi mitatu kwa muhtasari		14	Katika suuratul-baqara.
Sababu zina gawanyika kwenye		15	Ni mila iliyo mbali na shirki iliyojengwa katik ikhlasi na Tauheed.
Nadhiri imegawanyika kwenye		16	Ni kumpwekesha Allah kwa vile alivyojiita na kujisafisha katika kitabu chake na kwa maneno ya mtume wake swalla llahu alayhi wasallama na hayo ni mwenyewe na kukanisha yale aliyoyakanusha yeye mwenyewe bila ya kubadilisha wala kuzidishs na bila ya kufananisha .
Kunagawanyika kuchinja kwenye		17	Ni kumpwekesha Allah katika ibada
Kinagawanyika khofu			
Kinagawanyika khofu		18	Kumpwekesha Allah katika kuumba,kumiliki na kuendesha

kwenye		19	
Uslamu		20	Ni kumpwekesha Allah kwa yale ambayo yana muhusu.
Misingi ya dini		21	Ni asili ya kitendo(alifanya kitu kuwa kimoja)
Imani			Ni kuchomoza jua upande wa magharibi au kufikiwa na umauti.
Kuamini siku ya mwisho kuna fungamana		22	
Miongoni mwa Kujiweka mbali na shirki		23	Yale ambayo anavuka mja mipaka yake katika kuabudu au kufata au kutii.
Muda wa kukoma toba		24	Ni Tawhed ya majina na sifa au Tawheed ya uungu na kujiweka mbali na shirki.
Shetani		25	Ni kujisimamisha na Allah na kufuata kwa kutii na kujiepusha na shirki na watu wake.
			Kile kinacho abudiwa kinyume na Allah juu ya picha.

KUNAGAWANYIKA KUCHINJA KWENYE		17	NI KUMPWEKESHA ALLAH KWA IBADA
INAGAWANYIKA KHOFU KWENEYE		18	NI KUMPWEKESHA ALLAH KWA KUUMBA NA UFALME NA KUENDESHA .
UISLAMU		19	NI KUMPWEKESHA ALLAH KWA YANAYOMHUSU .
MISINGI YA DINI		20	ASILI YA KITENDO ALIPWEKESHA KITU . NI KUKIFANYA KITU KUWA KIMOJA .
IMANI		21	NI KUCHOMOZA JUA KUTOKA MAGHRIBI AU KUFIKWA MAUTI .
KUAMINI SIKU YA MWISHO KUNAFUNGAMANA		22	NI KUVUKA MTU MIPAKA YAKE KWA KUABUDU AU KUFATA KUTII .
KATIKA KUJIEPUSHA NA SHIRKI		23	TAWHEED YA MALEZI NA MAJINA NA SIFA NA TAWHEED YA UUNGU NA KUJIEPUSHA NA SHIRKI NA WATU .
WAKATI WA KUKOMA TOBA		24	NI KUJISALIMISHA KWA ALLAH NA KUFATA KWAKE KWA KUTII NA KUJIEPUSHA NA SHIRKI NA WATU .
SHETANI		20	NI KLE KINACHOABUDIWA KWA PICHA


AL-QAWAAIDUL-AR-BAA (KANUNI NNE)

BISMILLAH RAHMANI RAHIM

Kwa hakika kila sifa njema ni milki yake Allah. Tunamsifu na tunamuomba msaada. Na tunamtaka msamaha, tunajilinda kwa Allah na shari zote zitokanzo na nafsi zetu na ubaya wa matendo yetu. Yeyote ambaye ameongolewa na Allah basi hakuna yeyote atakae mpoteza, na Yule aliyempoteza hakuna wa kumuongoa.

Ninashuhudia ya kwamba hakuna anayestahiki kuabudiwa ila ni Allah pekee asiye na mshirika. Na namshuhudia ya kwamba Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake ni mja wa Allah na mtume wake. Ama ba'ada


Al-qaiwaidul-Ar-baa ndio matini ya pili ambayo imesomeshwa katika mfululizo wa matini za mtafuta Elimu. (mwanafunzi) umepatikana umuhimu wa kushughulikia matini hii kutokana na sababu nyingi sana. Miongooni mwazo ni:



Tutaianza hii matini kabla ya kitabu (kashfu shubhati,) ili isinase katika nafsi ya mwanafunzi shubha yeyote ile.

YALIYOMO KWENYE AL-QAWAAIDUL-AR-BAA

Imegawanywa hii matini katika sehemu tatu ambazo ni;



JAMBO LA KWANZA: UTANGULIZI

(ANUANI YA MAFANIKIO)

BISMILLAH RAHMAN RAHIM.

- (1) Namuomba Allah mkarimu
Mola mlezi wa Ar-sh tukufu
akupende Duniani na
Akhera
(2) Na akufanye kuwa ni
mbarikiwa popote
uwapo(3)

1. Sababu ya mtunzi kuanza matini yake kwa (Bismillah)

1. Kukiiga kitabu cha Allah na mitume na manabii, amani ya Allah iwafikie

2. Kwa kuwaiga walio kabla yake, katika wanachuoni wema ambao ilikua kawaida yao kuanza vitabu vyao kwa (Bismillah)

3. Ni katika mlango wa kutafuta Baraka kwa jina la Allah mtukufu.

Amesema Shaikhul Islami bin Taimiyya Allah amrehemu: (Atakae kuwa ni muumini mchamungu, atakuwa kipenzi cha Allah) dalili yake ni maneno ya Allah mtukufu: (Jueni kuwa vipenzi vya Allah hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika (62) Hao ni ambao wameamini na wakawa wanamcha Mungu)

BARAKA: Maana yake ni kukua na kuzidi

TABARRUKU: Maana yake ni kuomba kukua na kuzidia. (kuomba Baraka)

MUBARAKU: Maana yake ni Yule ambaye hupatikana manufaa kupitia yeye popote awapo. (alie barikiwa)

Na akujaalie miongoni mwa wale wanapo pewa humshukuru Allah (1)

KUOMBA BARAKA KUMEGAWANYIKA KATIKA SEHEMU MBILI

Kuomba Baraka kisheria

Kuomba Baraka kuliko katazwa. Huo ni uombaji ambao haikuthibiti chochote kisheria, wala kihisia na hiyo ni katika aina za shirki ndogo.

Ama kisheria. Mfano; kuswali ndani ya masjidil-haram (Makka) au masjidi Nnabawiy. Msikiti wa mtume (Madina)

Ama kihisia: Elimu au dua na vinginevyo mtu hutakwa Baraka kwa elimu alionayo na kwa kule kulingania kwake kwenye kheri, kwa hiyo hii inakua ni Baraka kwa sababu sisi tunapata kheri nyingi kutoka kwake. Mfano vitabu vya shaikhul- islam na wengine katika wanachuoni ambao Allah ametia Baraka na kheri katika vitabu vyao, na umma ukanufaika navyo.

- (1) Neema yeyote ni majaribio, pia ni mtihani. Dalili za hilo ni nyingi sana miongoni mwazo Allah anasema: (Na tunakujaribu kwa mtihani wa shari na kheri,) (Basi alipokiona kimewekwa mbele yake (kiti cha ufalme) akasema: Haya ni katika fadhila zake Mola wangu mlezi, ili anijaribu nitashukuru au nitakufuru Na mwenye kushukuru, kwa hakika anashukuru kwa manufaa ya nafsi yake, na anaye kufuru, kwa hakika Mola wangu mlezi ni mkwasi na karimu). (Ama mtu anapojaribiwa na Mola wake mlezi, akamkarimu na kumneemesha, husema: Mola wangu mlezi umenikirimu!) Na katika Hadithi (Hakika watatu katika wana wa Israili, Allah alitaka kuwajaribu.....)

**NEEMA NI ZENYE KUSHIKAMANA NA TAUHID YA MALEZI YA ALLAH. (RUBUBIYYA)
NA TAUHID YA IBADA (ULUHHIYYA) NAKUZISHUKURU KWAKE KUMEGAWIKA
VIGAWANYO VIWILI.**

Kushikamana na Allah kabla ya kupata neema

Na aina hii inamtaka mja aamini imani isiyo na shaka ya kwamba mwenye kutoa neema ni Allah swalalahu walayhi wasalam hivyo ushikamane moyo wake kwa asiekuwa Allah wala asitafute kheri kwa yeyote isipokuwa kwa Allah tu. Kama vile pepo hutafutwa kwa Allah swalalahu walayhi wasalam kwani yeye ndiye mmiliki wake, pia hata riziki haiwezekani kutafutwa isipokuwa kwa Allah tu. Allah anasema (Na mtegemee aliye hai ambaye hafi) hakika hao mnaowaabudu badala ya Allah hawakulimikini riziki yoyote.

Takeni riziki kwa Allah, yaani kutoka kwa Allah tu, na si kwa mwingine, na mumshukuru yeye na mumshukuru yeye.

Kushukuru baada ya kupata neema inakuwa kwa;

MOYO

Kwakuwa na imani ya kweli na kumuamini, na kujisalimisha kuliko timia ya kwamba anaeetoa riziki na kuneemesha ni Allah subhanahu wataala hakika kila neema aliyokuwa nayo mja inatoka kwa Allah subhanahu wataala


ULIMI

Hilo ni kwakuzungumza neema za Allah na kwa kusifu na kumshukuru juu ya hizo neema kwa kauli yake Allah mtukufu (Na neema za Mola wako mlezi zisimulie)

VIUNGO

Na hilo ni kwa kuzitumia neema kwa namna ambayo Allah subhanahu wataala ataturidhia, pia kwa kuongeza kufanya matendo mema kwa lengo la kujiweka karibu na Allah subhanahu wataala na kujiepusha na maasi. Kwa kutekeleza amri zake Allah.

1. HAKIKA SUBIRA NI WAJIBU KWA MAKUBALIANO YA UMMAA HUU.



1. **KUCHUKIA.** Ni jambo la haramu na ni katika madhambi makubwa na huwa kwa;



- **KUCHUKIA KWA MOYO.** Amesema Imaam Ibnul-qayyim Al-jauziyya. Katika maana ya maelezo yake, “hakika baadhi ya watu hawathubutu kuseema maneno haya kwa ulimi wao lakini nafsi yake ambayo ipo katika mwili wake hushuhudia hilo. Kwa kumdhania Mola wake mlezi dhana mbaya Husema kwa moyo wake, Mola wangu mlezi dhana mbaya Husema kwa moyo wake, mola wangu mlezi amenizuwilia. Kuna anaesema sana na anaesema kidogo. Kwa hiyo ichunguze nafsi yako, je wewe umesalimika na hii dhana? Ukiwa umeokoka nayo basi umeokoka katika jambo kubwa sana.”
 - **KUCHUKIA KWA ULIMI.** Inakuwa kwa kupiga kelele, na kunung'unika na kupiga mayowe, na kulaani na kutukana.
 - **KUCHUKIA KWA VIUNGO.** Inakua kwa kupiga mashavu na kuchana nguo, na kunyofoa nywele.
2. **SUBIRA.** Hukumu yake ni wajibu kwa makubaliano ya umma huu ni wajibu kuwa na subira katika moyo wake na ulimi wake na viungo vyake. Amesema Imaam Ahmad (Limekuja neon SUBIRA katika Qur'an karibu sehemu tisini kuwa na subira ni wajibu kwa makubaliano ya umma huu. Subira ni nusu ya iman, Kwani imani ipo nusu mbili. 1. Nusu ni kusubiri 2. Nusu ni kushukuru) Rejea kitabu (MADARIJUASSALIKINA) CHA Ibn-qayyim.
3. **KURIDHIA;** Hukumu yake ni mustahabu (Ni jambo lenye kupendwa) na hilo lina daraja ya juu kuliko subira.
4. **KUSHUKURU;** Hukumu yake ni mustahabu. (Ni jambo lenye kupendwa) na ndio daraja bora na kamilifu yake.

BISMILLAH RAHMAN RAHIM

Fahamu ewe Muislamu, Allah akuongoe kwenye twaa yake, Hakika uongofu wa kweli ni kufuata mila ya Nabii Ibraim (Amani ziwe juu yake) Nako ni kumuabudu Allah pekee hali ya kumtakasia dini yake, kwa sababu Allah ndio amewaamrisha watu wote (waifuata hiyo tauhid) na amewaumba kwa ajili yake. Kama alivyosema Allah:

“Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu mimi” (1)

Ikiwa umetambua kuwa dhumuni kuu la Allah kukuumba wewe ni kwa ajili ya kumuabudu yeye tu, Basi tambua pia kuwa ibada haitoitwa ni ibada ila iwe na tauhid ndani yake, kama ilivyo swala haiwezi kuitwa swala ila iwe na twahara, Basi shirki ikiingia kwenye ibada yoyote huiharibu kabisa ibada hiyo, kama vile hadathi inapoingia kwenye twahara (huiharibu)

- (1) Mwandishi Allah amrehemu anabainisha sababu za sisi kujifunza Tauhid.
- (2) Makafiri ambao mtume swalallah alayih wasalama alitumwa kwao walikuwa wakiikiri Tauhid rububiyya pamoja na hivyo mtume swalla llahu alayih wasallama aliwapiga vita. Ugomvi uliokuwa kati yao na mtume swalla llahu alayih wasallama ilikuwa ni Tauhid ya ibada, Basi kwa kila atakaye elekeza ibada yoyote kwa asiye kuwa Allah huyo atakuwa ni mshirikina kafiri.

Ikiwa umefahamu kwamba shirki inapochanganyika na ibada huiharibu, na huporomosha thawabu za amali hiyo na mwenye kutenda hilo atakuwa mtu wa motoni milele hapo utakuwa umefahamu kuwa lililo hapo wajibu kwako ni kujua Tauhid tu ili Allah subhanahu wataala akunasue kwenye huo mtego wa shirki, ambayo Allah ameisemea ndani ya Qur'an 4:48:

"Hakika Allah hasamehi kushirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye, Na anaye mshirikisha Allah basi hakika amezua dhambi kubwa sana"(1)

Na hilo la kujiepusha na shirki litafanikiwa kwa kuzijua kanuni nne ambazo Allah kazitaja ndani ya kitabu chake.

KANUNI YA KWANZA.

Ni kufahamu kwamba, makafiri mabao mtume subhanahu wataala alipigana nao walikuwa wakithibitisha kuwa Allah aliye tukuka ndiye muumbaji na ndiye mpangaji wa mambo yote, lakini imani hiyo haikuwafanya wao kuingia kwenye Uislamu. Dalili ya hilo ni kauli yake Allah subhanahu wataala

Sema: Ni nani anaye kuruzuku ni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Au ni nani anaye miliki kusikia na kuona? Na ni nani amtoaye hai kutoka maiti? Na akamtoa maiti kutoka aliye hai? Na nani anaye yapangilia mambo yote? Watasema: Allah. Basi sema: Je Hamumchi? (10:31) (2)

KANUNI YA PILI:

Makafiri husema: sisi hatuwaombi (hao) na kuwaelekea isipokuwa ni kwa ajili ya kufuta kurba na shafaa kutoka kwao.

Dalili ya kutafuta kurba ni kauli yake Allah subhanahu wataala

"Na wale wanaowafanya wenginewe kuwa walinzi wakisema: Sisi hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Allah – Hakika Allah atahukumu baina yao katika wanayokhitalifiana. Hakika Allah hamwongoi aliyemuongo kafiri (39:3) (1)

DALILI YA KUTAFUTA SHAFAA.

Nao badala ya Allah wanabudu wasio wadhuru wala kuwanufaisha na wanasema: Hawa ndio waombezi wetu kwa Allah! Sema: Je! Mnamwambia Allah asiyoyajua ya katika mbingu wala katika ardhi? Subhannahu wa Taa'la! Ametakasika na ametukuka na hao wanao mshirikisha naye. 10:18

SHAFAA (UOMBEZI) UKO WA NAMNA MBILI:

- 1- Uombezi unaokubalika
- 2- Uombezi usio kubalika. *2

**(1)* Makafiri na washirikina hujenga hoja ya kuwa wao hawaiombi na kuelekea Miungu yao ya batili isipokuwa ni kwa ajili ya kuruba na uombezi kutoka kwao kwa hakika walistahiki kwa hali hiyo mtume swalalahu walayhi wasalam awakufurishe na kuwapiga vita.

(2)* **SHAFAA: Kilugha ni kukusanya na kukifanya kitu kimoja kuwa viwili.

SHAFAA: Kisheria ni kumuweka kati kiumbe mwingine kwa lengo la kuleta manufaa au kuondoa madhara.

VIGAWANYO VYA SHAFAA

SHAFAA INAYOKUBALIKA.

Hiyo ni ile inayoombwa kutoka kwa Allah. na sharti zake ni kama ifuatavyo:

- 1- Ruhusa ya Allah kwa uombezi huo.
- 2- Ridhaa ya Allah kwa aneombea.
- 3- Ridhaa ya Allah kwa anae ombewa.

KWENYE MAMBO YALIYO KWENYE UWEZO WA KUIMBE.

Shafaa itafaa kwa sharti nne zifuatazo:

- 1- Muombezi awepo
- 2- Awe hai
- 3- Awe na uwezo juu ya jambo hilo
- 4- Awe ni sababu tu (Asiitakidiiwe ndio muwezeshaji)

SHAFAA ISİYOKUBALIKA:

Shafaa hii iliyokanushwa na Qur'an ni ile ambayo huombwa kwa asiye kuwa Allah katika mambo ambayo hakuna mwenye uwezo nayo ila ni Allah pekee. Hukumu ya shafaa hii ni shirki kubwa atakayeifanya.

Shafaa inayomuhusu mtume pekee wala hakuna anaye shirikiana nae katika hilo

Shafaa ya pamoja ya mitume, malaika, waja wema na watoto wadogo.

SHAFAA KUU

Shafaa kwa amini yake ABU TWALIBU apunguziwe adhabu

Uombezi wake mtume ili milango ya peponi ifunguliwe

Kwenye kuinua daraja za waumini

Kwa Yule aliyestahiki kuingia motoni asiingie motoni

Kwa Yule aliyeingia motoni katika waislamu atolewe humo

UOMBEZI USIOKUBALIKA:

Ni ule utakao kuwa unaombwa kutoka kwa asiye kuwa Allah subhanahu wataala kwenye mambo ambayo hakuna awezaye ila yeye tu. Na dalili yake ni kauli ya Allah subhanahu wataala;

“Enyi mlio amini! Toeni katika tulivyo kupeni kabla haijafika siku ambayo hapatakuwapo na biashara, wala urafiki, wala uombezi. Na makafiri ndio madhalimu. (2:254)

UOMBEZI UNAOKUBALIKA:

Huu ni ule ambao unaombwa kutoka kwa Allah, Lakini muombaji awe amekimiriwa huo uombezi na anayeombewa awe ni Yule Allah aliyemridhia kwa kauli na matendo baada ya kutoa ruhusa. Kama alivyosema Allah subhanahu wataala

“Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila idhini yake? (2:255).

KANUNI TA TATU: (1)

Hakika Mtume swalla llahu alayhi wasallama alikuja kwa watu waliokuwa wametofautiana katika ibada zao, miongoni mwao wamo waliokuwa wakiwaabudu malaika, Wengine wakiwaabudu mitume na watu wema, wengine wakiabudu miti na mawe, na wengine wakiabudu Jua na mwezi. Mtume swalla llahu alayhi wasallama hakuwatenganisha bali alipigana nao wate.

Ushahidi juu ya hilo ni kauli yake Allah subhanahu wataala

“Na piganeni nao mpaka isiwepo fitna na mateso, na dini yote iwe kwa ajili ya Allah.....(8:39)

DALILI YA KUABUDU JUA NA MWEZI NI KAULI YAKE ALLAH SUBHANAHU WATAALA:

Na katika ishara ake ni usiku na mchana, na jua na mwezi: Basi msilisujudie jua wala mwezi bali msujudieni Allah aliye viumba ikiwa nyinyi mnamuabudu yeye tu. (41:37)

*(1) Kanuni hii dalili ya wazi kabisa katika kuwapinga wale wote wanaosema kuwa shirki inakuwa tu kwa wale wanaoabudu masanamu zikaja dalili zote za kisheria kuhusiana na kuabudu masanamu na miungu mingine yote ya batili iliyokuwa ikiabudiwa kipindi hicho.

Wala mtume **swalla llahu alayhi wasallama** hakubagua kabisa kati ya miungu hiyo bali alihesabu miungu yote ni katika mataghuti, akapigana na wote wenye kuiabudu bila kumuacha hata mmoja ili dini yote iwe ni ya Allah subhanahu wataala isiyokuwa na hata chembe moja ya shirki.

NA DALILI YA KUABUDU MALAIKA NI AYA IFUATAYO:

Wala hatakuamrisheni kuwafanya malaika na manabii kuwa ni miungu.....(3:80)

NA DALILI YA KUABUDU MITUME NI KAULI YAKE ALLAH SUBHANAHU WATAALA

“Na pale Allah atakaposema: Ewe Isa bin Maryam! Ati wew uliwaambia watu: nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Allah? (Na Isa) atasema: Subhanaka, wewe umetakasika! Hainifai mimi kusema ambayo si haki yangu. Ikiwa nilisema basi bila shaka umekwisha yajua; Wewe unayajua yaliyomo ndani ya nafsi yangu, lakini mimi siyajui yaliyomo ndani ya nafsi yako. Hakika wewe ndiye mjuzi mkubwa wa yaliyofichikana. (5:116).

NA DALILI YA KUABUDU WAJA WEMA NI AYA HII?

Hao wanao waomba, wao wenyewe wanatafuta njia ya kwenda kwa Mola wao mlezi Hata miongoni mwao walio karibu mno – na wanataraji rehema zake na wanaikhofu adhabu yake. Hakika adhabu ya Mola wako Mlezi yafaa kutahadhari nayo (17:57)

NA DALILI YA KUABUDU MITI NA MAWE INAPATIKANA KATIKA AYA IFUATAYO:

Je! Mmemuona Lata na Uzza? (19) Na Manaas, mwingine wa tatu? (20) (53:19-20)

Na hadithi iliyoelezwa na sahaba ABU WAQID AL-LAYTH (Radhiyallah an’hu) amesema:-

“Tulitoka tukiwa na mtume swalla llahu alayhi wasallama kuelekea katika vita vya Hunaini (Baada ya Fatih – Makka)

Hali ya kuwa sisi ni wageni katika Uislamu, na washirikina zama hizo walikuwa wana mti wa mkunazi wakikaa itikafu kwenye mti huo na wakitundika silaha zao juu yake (kwa ajili ya kutabaruku) Mti huo uliitwa dhatu an-wati, tulipo upitia mkunazi nasi tukasema: Ewe mjumbe wa Allah! Nasi tuwekee mti wa kutundikia silaha zetu zibarikiwe kama wale washirikina wanavyofanya.....

KANUNI YA NNE:

Hakika washirikina wa zama zetu (za sasa) wana shirki kubwa zaidi kuliko wale wa mwanzo, kwa sababu washirikina wa mwanzo walifanya shirki kipindi cha raha na wakijitakasa kipindi cha shida. Lakini washirikina wa zama zetu shirki yao ni ya wakati wote kwenye raha na shida (huendelea na shirki zao)

Dalili ya hilo ni kauli ya Allah:

“Na wanapopanda katika marikebu humuomba Allah kwa kumsifia utiifu. Lakini anapo wavua wakafika nchi kavu mara wanamshirikisha (1) (29:67)

WALLAHU – A’ALAMU

(ALLAH NDIO MJUZI ZAIDI)

Rehema na Amani zimwendee Mtume wetu Muhammad yeye na jamaa zake na sahaba zake wote.

*Kwenye kanuni hii ya nne mwandishi “Allah amrehemu” ameweka wazi upeo wa hatari ya msimamo wa washirikina wa hizi zama zetu, wao ni washirikina wakubwa mno kuliko hata wale washirikina wa mwanzo, kwa sababu washirikina wa hizi zama tulizo nazo humshirikisha Allah subhanahu wataala katika shida na raha, ama washirikina wa mwanzo wao walimshirikisha Allah subhanahu wataala katika kipindi cha raha tu, na kipindi cha dhiki na tabu waliukiri upweke wa Allah subhanahu wataala wakamtakasia ibada.

Ikiwa washirikina ambao Mtume *swalla llahu alayhi wasallama* alipelekwa kwao, shirki yao ni ndogo ukilinganisha na zama hizi, lakini Allah subhanahu wataala aliwapinga na kuwakufurisha, Je hali itakuwaje kwa wale ambao shirki zao ni kwa wakati wote, kwenye shida na raha? Basi hao ndio wanastahiki zaidi kuwa makafiri (kuliko wale wa mwanzo).

YENYE KUFUNGAMANA NA TAUHID YA MALEZI	Kutafuta pepo hakuwi isipokuwa ni kutoka kwa Allah kwa sababu yeye aliyetukuka ndiye ambae anaimiliki, na hivyo hivyo Riziki haitafutwi ila kutoka kwa Allah. Basi hatuna budi kufungamana kwa Allah, na sio kwa Mwingine.	
	YENYE KUFUNGAMANA NA TAUHID YA IBADA	Kushukuru kwa moyo wake: kwa kujua na kukiri kuwa, hakika kila jambo lenye neema basi jambo hilo limetoka kwa Allah na sio kwa mwingine Kushukuru kwa kusema kwake. <i>(Haya ni katika fadhila zake mola wangu mlezi ili anijaribu nitashukuru au nitakufuru)</i> Kushukuru kwa viungo vyake: Ni kuitumia neema katika kumshukuru mwenye kuneemesha, na kila neema kwa kiwango chake, kwa hiyo kushukuru neema ya mali ni kuitoa katika Twaa ya Allah, na kushukuru neema ya elimu ni kuitoa kwa mwenye kuiomba, ima kwa kusema kiuhalisia au kimakala.
	HALI YA WATU WAKATI WA MATATIZO	Hasira: Hukumu yake ni kubwa bali inampeleka mtu kwenye shirki ndogo, na nakuwa na hasira kwa moyo, kuzungumza na kutekeleza Subira: Hukumu ya subira ni wajibu kwa makubaliano ya umma, husubiri mtu kwa moyo wake, ulimi wake, na viungo vyake na subira mfano wa jina lake imejipamba kutokana na utamu (asali).
KUSHUKURU NEEMA		
NEEMA NI MTIHANI ALLAH AMESEMA (NA TUNAKUJARIBUNI KWA MTIHANI WA KHERI NA SHARI)		
PINDI AKIPENDA HUSHUKURU		
ANWANI YA WEMA		
UTANGULIZI NA NDANI KUNA ANWANI YA MAFANIKIO		
KANUNI NNE NAYO NI UFUPISHO (KASHF-SHUBHAT)		

					RADHI: Hukumu yake ni yenye kupendeza (inastahiki) na kukamilika radhi zake kwa Mola wake ajue kwamba kila lile lililo mpata basi limetoka kwa Allah na kila lile alilokadiria Allah kwa mja wake KUSHUKURU: Ni jambo lililokuwa juu zaidi ya misingi nalo ni jambo lenye kupendeka zaidi na linakuwa jambo hilo kwa waja wa Allah wenye kushukuru
					PINDI ANAPOFANYA DHAMBI HUOMBA MSAMAHA.
				KWANINI TUNAJIFUNZA TAUHID NA HATARI YA SHIRKI?	HANIFIA: Mila ya Ibrahimu, Hakika Allah amekuumba wewe kwa ajili ya ibada yake (kumuabudu) Ibada yoyote haiwezi kuitwa ni ibada mpaka ibada hiyo iwe pamoja na Tawhid. Na pindi shirki ikichanganyikana na ibada huiharibu na kuporomosha amali za mja, na kumfanya mja huyo kuwa ni miongoni mwa watakaoishi motoni milele. Na ni mambo yaliyo muhimu zaidi juu yako kuyajua.
					MSINGI WA KWANZA: Hakika makafiri waliompinga mtume swalalahu walayhi wasalam walikuwa wanakiri Tauhid ya malezi, lakini walikuwa hawakiri Tauhid ya uungu. Jambo hili la kukiri halikuweza kuwafanya wawe waislamu.
					MSINGI WA PILI: Hakika Makafiri walikuwa wanaabudu masanamu kwa ajili ya maombi na kujikurubisha.
					MSINGI WA TATU: Hakika mtume aliwakuta watu wametofautiana katika ibada zake, na hakutofautisha kati ya shirki na shirki.
					MSINGI WA NNE: Hakika washirikina wa zama hizi, shirki zao ni kubwa kuliko shirki za watu waliotangulia.

MTIHANI WA KANUNI NNE.

JINA: _____ KIWANGO CHA KUHIFADHI KITABU CHA TAWHID _____

JE UMEHIFADHI MISINGI MINNE: _____

KAZI	DALILI KUTOKA KATIKA QUR'AN AU HADITHI.
NEEMA YA MTIHANI	
KUKIRI MAKAFIRI TAUHID YA MALEZI	
KUTAFUTA UKARIBU	
MAOMBEZI YALIYOKATALIWA	
DALILI YA JUA NA MWEZI	
DALILI ZA MALAIKA	
DALILI ZA MANABII	
DALILI ZA WEMA	
DALILI ZA MAWE NA MITI	
HAKIKA WASHIRIKINA WAKATI WA MATATIZO WANAMUAMINI NA KUMTAKA ALLAH WAKATI WA RAHA WANAMSHIRIKISHA.	
DALILI ZA SHIRKI	

ANDIKA KILE UNACHOKIJUA KWA YAFUATAYO:-

KWANINI TUNAJIFUNZA TAUHID	1-	2-	3-	4-
5-	6-	7-	8-	9-
KWANINI TUNAJIFUNZA MISINGI -4	1-	2-		
-3	4-			
INAGAWANYIKA MISINGI 4 KWENYE	1-	2-	3-	
MISINGI YA MUKHTASARI KWA KITABU				
KWANINI TUNAJIFUNZA KITABU (KASHFU SHUB-HAAT)				
ANWANI YA MAFANIKIO	1-	2-	3-	
“HANIFIA” NI				
FAIDA YA KUSOMA MISINGI				
VIPENZI WA ALLAH NI:-	AMESEMA SHEIKH WA UISLAMU			
NA DALILI JUU YA HAYO	NA KWA AJILI GANI?			
KUNAKUWA KUSHUKURU NEEMA PAMOJA NA MFANO				
	1-			
2-				
3-				

Vipi kunakuwa kufungamana kwa mja ?	
Hali za watu wakati wa matatizo pamoja na hukmu	
Shafaa kwa kilugha	Shafaa kwa kisheria
Inagawanyika Shafaa kwenye :	
Masharti ya Shafaa iliothibiti	
Na inagawanyika kwenye : 1- na	Na inagawanyika kwenye : na
2- na	Na inagawanyika kwenye : na
Msingi wa kwanza	
Msingi wa pili	
Msingi wa tatu	
Msingi wa nne	
Hukmu ya matendo pindi yatakapochangayika na shirki	Na Dalili

	YALIYOMO:	UKURASA
1.	UTANGULIZI	3
2.	JAMBO LA KWANZA MAMBO MANNE YA MSINGI	10
3.	JAMBO LA PILI MAMBO MATATU YA MSINGI	16
4.	JAMBO LA TATU UMUHIMU WA KUJIFUNZA TAUHID	20
5.	JAMBO LA NNE MISINGI MITATU	21
6.	JAMBO LA TANO HITIMISHO	50
7.	KINAAMBATANA NA(MUHTASARI WA SHERHE YA MATINI KATIKA SURA YA JEDWALI)	53
8.	MTIHANI WA MISINGI MITATU NA DALILI ZAKE	57

	YALIYOMO	UKURASA
1.	UTANGULIZI (NA NDANI YAKE KUNA ANWANI YA MAFANIKIO)	66
2.	JAMBO LA KWANZA KANUNI YA KWANZA	71
3.	JAMBO LA PILI KANUNI YA PILI	71
4.	JAMBO LA TATU KANUNI YA TATU	73
5.	JAMBO LA NNE KANUNI YA NNE	75
6.	JAMBO LA TANO KINAAMBATANA NA(MUHTASARI WA SHERHE YA MATINI KATIKA SURA YA JEDWALI)	76
7.	JAMBO LA SITA MTIHANI WA KANUNI NNE	78
8.	JAMBO LA SABA YALIYOMO	81